epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Alhamisi Machi 14, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581615
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



**SANCHO HATAKI KURUDI MAN UTD**

UKURASA 22



# Samia aanika msimamo wake halisi

UKURASA 2

- Hana kundi ndani ya CCM
- Anusa upigaji mkubwa serikalini
- Uvunjaji mikataba unagharimu nchi
- Angalizo kwa viongozi wajitathmini
- Kazi nzuri Ardhi, uchafu ni mwingi

UKURASA WA 4

**TPHPA KUNUNUA NDEGE MPYA KUDHIBITI NZIGE, KWELEA KWELEA**

## Utata kisheria dhamana ya mama anayedaiwa kumla nyama mwanawe

UKURASA 10

**Mbowe** abwagwa na waandishi wa habari mahakamani

UKURASA 3



**Bil.** 215/- zatengwa programu ya kusuka ubora wa elimu nchini

UKURASA 4



**CHADEMA** yamtosa Matiko mbio ubunge wa Tarime Mjini

UKURASA 10



## Mchungaji Mgogo aibuka na hoja nzito kikokotoo mafao

UKURASA 3

MICHEZO YANGA SC YAAHIDI KULIPIZA KISASI UK.24 KATUNI UK.6

# Samia aanika msimamo wake

Na Mwandishi Wetu

RAIS Samia Suluhu Hassan ameweka wazi msimamo wake kichama na kiserikali, akionesha hana wa kumkumbatia, mwelekeo wake mkuu ni kila mtendaji wake kuwajibika.

Katika ujumbe wa aina yake, unaobeba ishara ya itikadi ya uongozi wake, Rais Samia ametumia fursa hiyo kutoa tahadhari ya kiutendaji kuanzia kwenye chama chake, Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambako yeye ni mwenyekiti hadi serikalini akiwa na itikadi 'mimi ni mtu wa wote'.

Ilikuwa kwenye tukio la jana la kuapisha viongozi mbalimbali aliowateua hivi karibuni serikalini, akiwamo aliyekuwa Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, anayekuwa Mkuu wa Mkoa wa Songwe na naibu wake, Anamringi Macha, katika cheo kama hicho mkoani Shinyanga.

Kauli hiyo ya kipekee ya Rais Samia aliitoa Ikulu katika hilo, ambalo mbali na wakuu wa mikoa, pia alikuwapo Christina Mndeme ambaye anakuwa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira).

Rais alitafsiri kwa kina msimamo wake kiutendaji na nyendo za kuwajibika kwa watendaji wote serikalini, hasa wanaowajibika kwake moja kwa moja.

Katika hotuba yake, Rais Samia aliweka wazi sababu za uteuzi wa kila mkuu wa mkoa na kutoa maelekezo mahususi na ya jumla kwa wateule wote, akiwa na msisitizo amewateua pasi na kuangalia makundi waliyonayo.

"Mabadiliko hayo wengine wamehamishwa na kuondolewa na si kwa kulenga mtu, bali kupanga safu nzuri kuelekea mbele. Wale mliobadilishwa nendeni mkasome vituo vyenu vipya, na uende inavyotakiwa.

"Wakati mwingine uliyebadilishwa ni kwa sababu ulipokuwapo changamoto ni chache, tunakupeleka kwenye (changamoto) nyingi tukiamini unaweza. Wakati mwingine ni nyingi na wewe ni mwepesi, tunampeleka ambaye ataweza. Ni mabadiliko ya kawaida, nendeni kufanya kazi.

"Mwanzo nilipoanza kuwaapisha wakuu wa mikoa niliwaambia mnatarajia ningewachagua kwa makundi, lakini mimi kama Samia sina kundi.

"Mkijitizama humo, makundi mnayoyajua wote mmo humo ndani, ninachotaka mimi Watanzania kwa pamoja tufanye kazi, tusogeze nchi yetu mbele, sina kundi. "Sasa wale wanahoji 'identify' (kujitambulisha) huyu ni wa mama huyu siyo wa mama, mimi mama nina watoto wote, wote wangu ninalea. Anayefanya vizuri wangu, anayefanya vibaya wangu, mwingine nitampa zawadi na mwingine nitamchapa mikwaju.

"Na wapo ninawachapa, ninawaweka nje, akishapata adabu yake ninamwambia njoo tufanye kazi. Kama makundi yenu huko, mimi hayanihusu, ninataka tufanye kazi 2024 na 2025 tuvuke vizuri," alisema.

**KUVUNJA MIKATABA**

Rais Samia pia alitoa angalizo kwa viongozi kutumia vibaya nafasi zao kwa kuvunja mikataba kwa njia ambazo si za kisheria na hivyo kusababisha serikali kushtakiwa na kuingia gharama kubwa za kulipa fidia.

"Tunalipa fedha nyingi sana kwa kuvunja mikataba ovyo, mtu hajawekeza hata shilingi kanyang'anywa ardhi, unaletewa bili hiyo 'lipa umekiuka Katiba na sheria, Dola 300 lipa'.

"Uvunjaji mikataba ufuate taarifa, vinginevyo DC (mkuu wa wilaya) na RC (mkuu wa mkoa) mnatutia hasara sana. Inawezekana umeenda mahali mtu anaudhi, lakini fuata taratibu kuvunja. Wengine ni matapeli kaingia, kategesha anakukasirisha ili afanye yake," alifafanua.

**WASIOWAJIBIKA**

Rais Samia alisema kuwa kila mwezi anapokea ripoti ya utendaji wa kila kiongozi, akibainisha kuwa vipimo vya wakuu wa mikoa ni pamoja na kuongeza mapato.

"Wizara ya Fedha walinipa taarifa ya mapato, matumizi na madeni na kuonesha makusanyo ya serikali ni asilimia 97.7, lakini TAMISEMI makusanyo yako kwenye asilimia 60 hadi 70 kwa baadhi ya halmashauri na nyingine ziko kwenye 50, lakini 15 ziko chini ya asilimia 50 na kuwataka wajitazame namna ya kupandisha.

"Katika kupandisha makusanyo si kwenda kuwabinya wananchi, kuna maeneo mengi yameachiwa zinaweza kukusanywa. Tunakwenda kupunguza kwa ajili ya huduma za kijamii; elimu, afya na maji, ili fedha zirudi TAMISEMI, lazima kukusanya.

"Ninataka mkasimamie mifumo ya ukusanyaji, watu wanaiba fedha, watu wote, RC, DC mpo? Kuna mitandao inachepusha fedha za halmashauri, mkoa, kuna mtandao wa serikali unakwenda sambamba na wa wizi, watu mpo mnaangalia. Ninashukuru Mbeya wamekuwa wa kwanza kutuambia, tumeona hebu angalieni na kwingine, tunafuatilia.

"Mtandao upo na unaenda, wanaambizana na unachepusha fedha nyingi sana. Lakini mnakaa huko 'barabara zimeharibika El-Nino tunaomba fedha hizi', zinatoka wapi? Serikali hatuchapishi fedha, bali tunakusanya kodi huko na huku kwenu mkiziachia zipotee hizi za huku zitazidiwa, tuna miradi mikubwa ya kitaifa, kuna mabwawa, reli.

"Huko kwenye huduma za kijamii tumefanya vya kutosha, sasa tunakwenda kupunguza fedha labda mkusanye. Lakini halmashauri zitapewa fedha kutokana na makusanyo yake na watapewa kwa kadri ya kukusanya, wakipiga kelele nitafanya tathmini ya utendaji wako (kiongozi)," alihadharisha.

**MIGOGORO YA ARDHI**

Rais Samia alisema migogoro ya ardhi imekuwa mingi, watu hawana raha, kuna wababe wanajifanya maofisa ardhi wanawanyang'anya, akiagiza viongozi kusimamia haki za watu.

"Ninafurahishwa na juhudi za sasa za Wizara ya Ardhi kupita, kusikiliza kero na kuzitatua palepale, lakini waziri ni mmoja na timu yake wanaburuza wanakwenda, angalau wameanza na hawawezi kwenda kila mahali, bali serikali (viongozi) wafuatilie.

"Wakati huu tulionao uchaguzi wa serikali za mitaa ndio wakati wa kusababisha migogoro ya ardhi, mtu akiona ameharibu upande mmoja, anajenga mazingira linakatwa eneo anajisogeza na kijiji kinasajiliwa na wakifanya tathmini hakikuwapo na kimesogezwa kwenye hifadhi, wilaya au mkoa mwingine.

"Ramani zilivyokuwa kipindi kilichokuwa wakati wa uchaguzi hakuna kuongeza kijiji wala nini. Huu ndio mtindo wa madiwani, wakishavurunda huku wanakata upande mwingine, nendeni kasimamieni," aliagiza.

Pia aliwataka viongozi hao kuchunga ndimi zao kwa kuwa wakati mwingine zinachangia migogoro ambayo ni kuminya haki za watu, watambue wako kwa ajili ya kusimamia haki za watu.

**MIKOPO YA 10%**

Rais Samia pia alisema suala la mikopo ya halmashuari wanaendelea kulimalizia ili kuwa na utaratibu mzuri, watu wasipate shida. Alisema kuwa katika mwaka huu wa fedha (2023/24) kuna fedha ilishaidhinishwa, ipo kwenye mfuko ikisubiri muundo mpya.

Alisema makusanyo yanapaswa kuendelea na ni lazima wadaiwa sugu washughulikiwe, lakini akawa na angalizo kwamba itafika mahali watashindwa kwa sababu waliochukua fedha ni madiwani na wenyeviti wa halmashauri ambao waliunda vikundi feki vilivyopewa majina na kuundiwa miradi hewa na kupewa fedha.

**SUKARI, MIGOGORO**

Mkuu wa Nchi pia aliwataka wakuu wa mikoa kushughulikia aliowaita "watukutu" na kuacha kula nao ili kusaidia wananchi wapate sukari. Kama kuna mkoa bidhaa hiyo haipatikani na ipo nchini, watakutana kwenye tathmini ya mwezi.

"Ninapata taarifa za ajabu ajabu, nyingine mnajihatarishia maisha wenyewe. Mungu awalinde. Jitambueni. Uhusiano mwema sehemu ya kazi, mimi ninashangaa RC na DC haziendi huyu na huyu, kama binadamu kila mtu alizaliwa kwao na makuzi ya kwao ila wote tumepita shule.

"Kama ya nyumbani hayaendani na uliyemkuta, basi angalieni yale ya jumla, mnagombana kwa kipi? Ukifuatilia ni mamlaka, fedha na mali ndivyo wanavyogombania.

"Wabunge wakija na hayo huwa ninawaambia 'hapana'. Kama unafanya vizuri jimboni kwako hakuna wa kukuondoa, kama hufanyi vizuri unataka kubebwa hilo halipo.

"Ila kuna visa RC anampangia mwenzake mbunge mwingine badala ya kumwita ambaye hamwendi vizuri na kuelezana maeneo ya utawala, kuna ambao hawataki kusimamiwa na wanaojiingiza kwenye yasiyowahusu," alionya.

**RC NI RAIS**

Rais Samia alisema lengo ni kuwakumbusha dhamana waliyonayo ni kwa kuwa mkuu wa mkoa ni mwakilishi wa Rais katika kipande cha ardhi alichoko, kwa maana ndiye Rais wa huko.

"Rais wa Tanzania mvua ikinyesha hukuna usingizi, unajiuliza wananchi wangu wa wapi wataamka wamezama, wapi nitasikia daraja limeporomoka, jua likitoka hulali je, wakulima watapata chakula? Vyanzo vya maji viko salama kweli, na ninyi mnatakiwa kuwa hivyo.

"Nimeona visa vingi hadi aje waziri mkuu azunguke huko akafungue maghala yaliyofungwa na RC mpo, na ninyi mnawaapisha DC ambao wamekatiwa kipande cha ardhi, lakini mambo hayaendi. Ninawakumbusha ninyi ndio marais wa eneo lile, shida yoyote ni yako," aliagiza.

**MTWARA**

Rais Samia alisema amempandisha cheo Kanali Patrick Sawala kutokana na kazi nzuri aliyofanya akiwa mkuu wa wilaya, huku akibainisha kuwa Mkoa wa Mtwara unapakana na nchi jirani, hivyo ahakikishe wanafanya vikao vya kujadiliana kupunguza changamoto za mpakani na kukuza biashara baina ya pande zote.

"Nenda kasimamie uzalishaji wa zao la korosho, mtangulizi wako alifanya vizuri, lazima kusimamia usafirishaji, tumeamua korosho yote isafirishwe kutoka Bandari ya Mtwara hatujapata lawama kwenye soko la dunia, tunapoamua korosho ije Dar es Salaam kuna mambo mengi yanafanyika, ila ikisafirishwa moja kwa moja tunapeleka zao lenye sifa,"alisema.

Aliongeza kuwa serikali imeanzisha kongani ya zao la korosho na ni muhimu kusimamia vyema ili kutoa ajira kwa wingi, huku akieleza bei nzuri ya zao mbaazi na ufuta inapaswa kwenda sambamba na usimamizi mzuri wa serikali.

**TABORA**

Alisema amemtoa Paul Chacha kutoka mkuu wa wilaya kuwa mkuu wa mkoa kutokana na kufanya vizuri huku akimtaka asimamie vyema mazao ya kilimo, hasa tumbaku na pamba pamoja na kutatua changamoto ya uharibifu wa mazingira.

Pia alimwagiza kusimamia zao asali ili wananchi wapate ajira na kusimamia mradi wa umwagiliaji eneo la Nala ili wananchi waachane na kilimo duni ndani ya mkoa huo.

Alisema TAMISEMI inatathmini wakuu wa mikoa na wilaya ili kujua wanaofanya vizuri na wanaofanya vibaya. Kwa Chacha, ripoti nzuri ilitolewa na ndio sababu wamempandisha.

**SONGWE**

Rais Samia alisema Chongolo anaijua vyema Songwe na matatizo yaliyoko huko tangu akiwa CCM. Inaunganisha nchi na Zambia kupitia Mpaka wa Tunduma ambako kuna shughuli nyingi za kiuchumi na uhalifu wa kiuchumi kama ukwepaji kodi, ubadilishanaji fedha isivyo halali.

"Kuna DED wa upande ule mzuri kaongeza mapato ya serikali, nenda kasaidiane naye pale Tunduma panaweza kuendesha mkoa na mkachangia serikali. Kuna matatizo ya TRA (Mamlaka ya Mapato Tanzania), nenda kawasaidie wafanye kazi zao vizuri wakiwa pale.

**SHINYANGA**

Mkuu wa Nchi alisema Anamringi Macha ana uzoefu mzuri ndani ya chama na maeneo mengine, ametulia na amekua; atafanya kazi nzuri, akimtaka kusimamia vyema uzalishaji pamba na kupandisha ari ya wananchi kujiletea maendeleo.

"Pale (Shinyanga) kuna mabwanyenye, kulalalala kidogo, kuna jamaa zangu wengi waarabu kidogo, wengi kazi 'mzigo mzito mpe mnyamwezi' ila sio wengine , nenda kasimamie watu wapate ari ya kufanya kazi na kujiletea maendeleo, kufuatilia kongani ya Buzwagi hasa kwa madini, hatujawahi kuwa na ya aina hii, nenda kaisimamie iwe na mafanikio," aliagiza.

**WALIOHAMISHWA**

Rais pia alisema Ruvuma hakuna changamoto nyingi kama Mtwara ila wakikosa mbolea, ikizingatiwa kuna tatizo la kiusalama mpakani, inakuwa shida.

"Ninadhani damu ya Peter (Serukamba) kule Singida haikuiva vizuri sana na viongozi walipo, vineno vineno vingi, nikijua Peter ni mtendaji mzuri sana, alikuwa anajaribu kurekebisha mambo wengine hawataki kurekebishwa, nikaona nikimwacha twende naye mpaka kule mbele kwenye kazi zetu zile, wanaweza kuharibiana.

"Halima (Dendego) wewe ni mama unaweza kulea, pale kuna watu wa kuelelewa kama ninavyowalea ninyi, nawe nenda kalee Singida, Singida ni ndogo lakini ina mambo yake," alisema.

Rais Samia alisema Serukamba anakwenda Iringa ambako kuko vizuri, hakuna changamoto nyingi na anadhani ataelewana nao vizuri; akiona anakwazwa amtafute Mtaka jirani yake (Mkuu wa Mkoa wa Njombe) atamwonesha njia ya kupita.

Kwa upande wa Balozi Batilda Buriani, Rais Samia alisema aanaamini atakwenda nao vizuri, akisisitiza kuwa waziri alikuwa anatumia nguvu, "mnyapara sana" na kumtaka asikubali wamwendeshe, lakini usibishane na wananchi wa Mkoa wa Tanga alikohamishiwa, bali asimame nao vizuri.

HABARI KITAIFA

# Mbowe abwagwa na waandishi kortini

**Na Mwandishi Wetu**

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Divisheni ya Kazi imetupilia mbali maombi ya Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe kutaka waandishi wa habari 10 wanaomdai mtoto wake, Dudley Mbowe wamlipe gharama kwa kukamata nyumba yake.

Uamuzi huo ulitolewa jana mbele ya Naibu Msajili wa Mahakama Kuu, Mary Mrio, baada ya kupitia hoja za pande zote mbili.

Akisoma uamuzi huo, Mrio alisema mahakama baada ya kupitia maombi yaliyowasilisha na Mbowe kupitia wakili wake, John Mallya, iliona kwamba hakuna ubishi katika maombi ya kuiachia nyumba. Alisema kinachobishaniwa mahakamani ni Mbowe kulipwa gharama za kesi na wajibu maombi.

"Mahakama iliangalia katika kesi hii gharama zilipwe au zisilipwe, nimepitia gazeti la Serikali (GN) namba 106 la mwaka 2007 ilielekeza kwamba kesi za aina hii hakuna sehemu inayoelekeza kulipa gharama.

"Mahakama inaona hakuna haja ya kutoa gharama, kila upande ubebe gharama zake, nyumba iliyokamatwa iko huru," alisema Msajili Urio.

Juzi waandishi wa habari 10 wanaomdai Mkurugenzi wa Tanzania Daima, Dudley Mbowe, Sh. milioni 62.7 waliachia nyumba ya Freeman Mbowe waliyoikamata ili kuipiga mnada, lakini waligoma kulipa gharama za kesi kwa sababu hata wao wanaingia gharama katika kudai haki yao.

Mbowe kupitia Wakili Mallya aliwasilisha maombi chini ya kiapo kilichoapwa na Freeman Mbowe, Februari 26 mwaka huu akitaka wajibu maombi kuondoa nyumba hiyo kwa sababu si mali ya Dudley na Mahakama iwaamuru wajibu maombi hao kumlipa gharama za kesi mteja wake.

Wajibu maombi kupitia mwenzao, Kulwa Mzee, walidai walipitia nyaraka zote na viambatanisho walijiridhisha na walikubaliana kwa pamoja kwamba hiyo nyumba waliyoikamata ni ya familia lakini inamiliiwa na Freeman Mbowe.

"Kuhusu gharama mheshimiwa, kwa uelewa wetu kwa mashauri ya migogoro ya kikazi hakuna gharama na hiyo inatokana na uwezo wa vipato vidogo vya wafanyakazi.

"Wakati sisi tunafanya hili jambo tulikuwa tukiamini kabisa kuwa ni nyumba ya mkurugenzi wetu kwa sababu katika hatua ya makubaliano alikuwa anatuambia kuwa tutafanya vikao nyumbani kwake na tumefanya hapo vikao kwenye hiyo nyumba.

"Mheshimiwa katika hatua za mwisho baba yake ambaye ndiye mwombaji katika shauri hili alitualika tukutane hapo hapo ambapo tulikuwa tunakutana na tulikutana hapo akakubali kubeba dhamana ya mtoto wake akakubali kutulipa mwezi Desemba," alidai Kulwa.

Kulwa alidai kutokana na mazingira hayo waliamini kuwa hapo ndipo nyumbani kwake mkurugenzi na baada ya kushindwa kuwalipa katika kutekeleza namna ya kupata haki yao ndio maana waliamua kukamata hiyo nyumba.

""Kwa hiyo mheshimiwa tunaomba tusilipe gharama. Kwanza, huyu mwombaji hajaingia gharama kwani katika hatua zote za majadiliano tulikuwa tunakwenda kwake kwa gharama zetu wenyewe na ahadi zake za kutulipa Desemba baada ya kushindwa kutekeleza hilo lilituathiri maana tulikuwa katika maandalizi ya siku kuu na ada za watoto shuleni," alidai Kulwa.

Kulwa aliomba Mahakama katika uamuzi kuhusu gharama ikiwezekana kila upande ubebe gharama zake.

Akijibu Wakili Mallya alidai anakubaliana na mjibu maombi Kulwa kwa aliyoyasema ya kuachia nyumba hiyo.

"Kuhusu suala la gharama mteja mwombaji anastahili kulipwa gharama na mambo mengine aliyoyasema mjibu maombi alipaswa kuyaleta kwa njia ya kiapo,"alidai Mallya .

Mbowe alifungua shauri dhidi ya Maregesi Paul, Fidelis Felix, Christina Mwakangale, Janeth Josiah, Exuperius Kachenje, Hellen Sisya, Kulwa Mzee, Nora Damian, Makuburi Ally, Mkurugenzi wa Gazeti la Tanzania na Kampuni ya Udalali ya JJ Auctioneers& Debt Collectors.

Februari 13, mwaka huu, Mahakama ilikubali maombi ya wadai na kumteua dalali wa Mahakama kukamata nyumba kwa ajili ya kuipiga mnada.

Februari 28, mwaka huu, dalali wa Mahakama, Jesca Massawe, alibandika matangazo ya kukamata nyumba ya Mkurugenzi tayari kupigwa mnada kufidia deni la malimbikizo ya mishahara ya wafanyakazi.

Naibu Msajili Mrio alitoa amri hiyo baada ya kupitia hoja za washinda tuzo katika Tume ya Usuluhishi na Uamuzi (CMA) Julai 2023.

Shauri hilo namba 28461 la mwaka 2023, wadai Maregesi Paul na wenzake tisa dhidi ya Mkurugenzi wa Gazeti la Tanzania Daima, Dudley Mbowe.

Baada ya mdaiwa kukaidi kulipa, wadai walikubaliana njia sahihi kukamata nyumba yake namba 9 iliyopo Mtaa wa Feza , Mikocheni B barabara ya Chipaka na Mahakama ilikubali.

Walalamikaji hao walipata tuzo Julai 17 mwaka 2023 mbele ya Msuluhishi wa CMA Ilala, Bonasia Mollel.

Madai ya awali yalikuwa jumla ya Sh. milioni 114 baada ya kukaa mezani kwenye majadiliano kwa pamoja kiwango hicho cha fedha kilishuka na kufikia Sh. milioni 62.7.

Dudley alikubali kulipa fedha hizo kwa awamu tatu, Oktoba 30, Desemba 30 mwaka 2023 na awamu ya mwisho ilikuwa mwishoni Februari mwaka huu lakini hakulipa.

# Mchungaji Mgogo aibuka na hoja nzito kikokotoo mafao

**Na Joyce Lameck**

KASISI machachari nchini, Mchungaji Daniel Mgogo, amesema kikokotoo bado ni maumivu kwa wastaafu kutokana na kuambulia kiasi kidogo cha mafao licha ya kutumia muda mwingi katika utumishi.

Kutokana na hali hiyo, amesema ni muhimu serikali ikaangalia upya suala hilo huku akishauri pia taratibu za mtu kupata stahiki zake zisiwe na usumbufu kama ilivyo sasa.

Akihojiwa katika channel ya Pastor Daniel Mgogo, alisema Mchungaji Mgogo alisema anaamini kama wabunge wangekuwa katika mfumo wa kikokotoo wasingekipitisha ndiyo maana hawapati maumivu katika mafao yao pindi wanapomaliza muda wao wa ubunge.

"Naamini kama hiki kikokotoo kingewakokotoa na wabunge wasingekipitisha. Nasema huwezi kuwapa kazi ya kutunga sheria ya barabara madereva bodaboda au magari maana watabadili mwendo na kila kitu watajiangalia wao. Nashauri tunapotunga hizi sheria wanasiasa wasiwapo," alisema.

Mchungaji Mgogo alisema anaamini kama bunge wangepitia kikokotoo wasingekipitisha na kwamba atauliza rafiki zake (wabunge) kama nao kinawahusu kwa kuwa kwa hali ilivyo wasingepaswa kukipitisha.

"Naamini kama hiki kikokotoo kingewakokotoa na wa bunge wasingekipitisha, ndio maana nasema huwezi kuwapa kazi ya kutunga sheria ya barabara madereva bodaboda au magari maana watabadili mwendo na kila kitu wakijiangalia wao. Nashauri tunapotunga hizi sheria wanasiasa wasiwepo.

Mchungaji Mgogo alisema mfanyakazi anapokuwa kazini anaamini kuwa pesa anayoiweka itamsaidia mara baada ya kustaafu, lakini imekuwa tofauti kwa watu wengi kwa sababu mzunguko wa kupata kikokotoo umekuwa mrefu.

Alishauri kuwa mtu kabla hajastaafu apewe barua ikiwa imeambatana na hundi na kama hakuna fedha basi aendelee na kazi hadi fedha zitakapopatikana.

"Kwa nini wanashindwa kuweka hundi? Kwa sababu wanataka wakuzungushe hadi ufe na unapofariki (dunia) ndugu zako waanze kuzungushwa hadi wakose stahiki hizo.



"Kama kuna kitu Watanzania wanataka kibadilike ni hili la kikokotoo. Ni jambo linaloulizwa sana. Serikali inaposema ukomo wako wa kufanya kazi umefika, pale wanapoweka ukomo na hundi yako iwapo badala ya nenda halafu baadaye unajaza fomu kuomba fedha zako.

Ili kuondoa huu usumbufu huo, alishauri mlolongo uondolewe na kuweka angalizo kuwa walioko kazini wajue ni wastaafu wa baadaye kwa sababu hawatafanya kazi milele na kwamba usumbufu wanaowafanyia wengine watakutana nao.

"Kinachonisumbua mtu kashatumika. Alikuwa akifanya kazi akilipwa mshahara. Anapostaafu kwa nini mnampa kazi ya kujaza fomu? Inatakiwa apewe fomu kwamba ulikatwa hivi na sasa unachostahili ni hiki, siyo kuanza kujieleza wakati 'database' (kanzidata) ipo na inaonyesha makato yake kwa miaka 30.

"Hali hii imesababisha mstaafu anageuka ombaomba barabarani wakati ni haki yake wakati kuna database ambayo inaweza kuondoa usumbufu kwa wastaafu kujaza fomu mara kwa mara huku wengine wakitoka vijiji vya mbali,"alisema.

Kwa mujibu wa Mchungaji Mgogo, hakuna haja ya mstaafu kuanza kujaza fomu upya ya kujielezea kwa kuwa ni mfanyakazi ambaye anajulikana na utumishi wake unajulikana katika sehemu yake ya kazi.

"Ni kwa nini muda unapofika wa kumpa kile ambacho walikuwa wanamtunzia ndio wanaanza kumpiga danadana? Mara tutakuwa tunakulipa kidogo kidogo tena kwa muda ambao watapenda wao. Hii si nzuri kabisa kuna jambo limejificha.

**WAKIMBILIA KUOMBEWA**

Mgogo alisema anaumia sana kwa sababu wastaafu wengi hivi sasa wanakimbilia nyumba za ibada kuomba kuombewa ili walipwe stahiki zao, jambo ambalo halipaswi kuwa hivyo kwa kuwa fedha zao zilishakatwa, hivyo wanapaswa kulipwa.

"Napokea simu za wastaafu wakisema Mchungaji naomba uniombee pesa yangu wanizungusha. Hivi fedha ya mtu ni ya kufanyia maombi kweli? Tuache kukemea mapepo na magonjwa, tukemee kikokotoo? Unamchelewesha babu wa watu amesharudi kijijini lakini haki yake haumpi," alihoji.

Aidha, alishauri vyama vya wafanyakazi kupeleka msimamo kwa serikali kama haina fedha isiwe inawastaafisha watu kwa kuwa ni mateso baada ya kutumikia taifa kwa miaka mingi.

**UJUMBE MZITO**

Kasisi huyo alitoa wito kwa Watanzania wanapopata nafasi yoyote ya kuwa juu ya watu wengine, wawe na moyo wa huruma katika kuwahudumia kwa sababu Mungu anapompa mtu kibali hicho, anaamini kuwa ana uwezo wa kusimamia na kuwasaidia watu wengine.

"Kila unachokifanya kwa mtu kigeuze kwa upande wako ili uone uhuruma kwa mtu huyo. Kwa sehemu ndogo Mungu aliyokupa ujisikie amani mtu anapoondoka akiwa amefurahi kwa kumuhudumia vizuri," alisisitiza.

**CHANZO CHAKE**

Mwaka 2018, serikali iliwasilisha kusudio la kubadilisha kanuni za Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa ajili ya kuweka kikokotoo kipya cha mafao kutoka asilimia 50 kwenda 25 ya mkupuo na hatimaye Bunge kusitisha.

Hatua hiyo ilisababisha wadau kuipinga kila kona, hivyo kumfanya Rais wa Awamu ya Tano, Dk. John Magufuli (marehemu) kusitisha matumizi ya kikokotoo kipya hadi mwaka 2023. Mabadiliko yalipelekwa bungeni na kubadilisha kutoka asilimia 25 hadi 33.

Hata hivyo, kikokotoo hicho badi kinapingwa huku wadau wakibainisha kuwa hakiakisi hali halisi ya maisha ya mstaafu kutokana na thamani ya utumishi wake kwa taifa na kile anachoambulia baada ya kustaafu.



Wavuvi wa pweza kutoka vijiji sita vya kata ya Boma, wilayani Mkinga mkoani Tanga, wakiwaandaa kwa ajili ya kuwapima ili kuwauza, wakati wa kufungua mwamba wa makazi ya samaki hao jana, ambao ulifungwa kwa siku 90 ili wazaliane ambapo kilogramu 2,284 zilivuliwa. Zoezi la ufungaji wa miamba bahari kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa pweza linasimamiwa na Shirika la Mwambao Coastal Community Network Tanzania chini ya mradi wa NORAD. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# TPHPA kununua ndege mpya kudhibiti nzige, kwelea kwelea

**Na Christina Mwakangale**

MAMLAKA ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA), imesema inatarajia kununua ndege mpya ya Shilingi bilioni tatu, kuongeza ufanisi katika udhibiti wa nzige na ndege jamii ya kwelea kwelea.

Imesema hatua hiyo ni mikakati ya TPHPA ya kuimarisha 'Kilimo Anga' na kwamba zitanunuliwa ndege zaidi ikiwamo ndege isiyo na rubani (drone), ili kudhibiti visumbufu mimea kama vile 'Kantangaze'.

Mkurugenzi Mkuu wa TPHPA, Prof. Joseph Ndunguru, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na wahariri na waandishi wa habari nchini, kuelezea mafanikio, changamoto na matarajio ya mamlaka hiyo mwaka 2023/24.

"Mamlaka imedhibiti ndege aina ya kwelea kwelea milioni 40 na kufanikiwa kuokoa tani 5,675 za mazao ya nafaka (mpunga, mtama na alizeti).

"Udhibiti huo ulifanyika katika mikoa ya Pwani, Morogoro, Tabora na Manyara kwa kushirikiana na Shirika la Kudhibiti Nzige wa Jangwani (DLCO-EA)," alisema Prof. Ndunguru.

Kadhalika, Prof. Ndunguru, alifafanua kwamba katika kudhibiti visumbufu mimea, njia tofauti za kisasa kiteknolojia kwa kutumia ndege zisizo na rubani, hutumika huku mwezi Februari na Machi, mwaka huu mradi wa BBT (Building a Better Tomorrow), ukifikiwa.

Alisema kwenye mradi huo, eneo la Chinangali, mkoani Dodoma, mamlaka imedhibiti visumbufu vya zao la alizeti (aphids, viwavi na panzi) katika eneo la ekari 495 za shamba la zao hilo.

"Udhibiti huo unafanywa na mamlaka kwa kutumia drone, ambayo ilinyunyuzia kiuatilifu aina ya Bamidacy Plus 344SE kwa ufanisi mkubwa na hivyo kuchangia kuokoa upotevu wa zao hilo, na kuchangia katika kuongeza tija.

"Tunatumia 'Ndege nyuki' (kifaa kama drone kwa njia ya anga), imechangia katika kupunguza gharama za uzalishaji ambazo zingetumika kuwalipa vibarua na kuokoa muda ambao ungetumika kufanya kazi hiyo, kama ingefanywa na vibarua.

"Ndege waharibifu hao walidhibitiwa katika maeneo yaliyotajwa kwa kunyunyizia kiuatilifu aina ya 'fenthion' kwa asilimia 60 kwa kutumia ndege na 'Vinyunyizi Mbeleko' vyenye injini (njia ya ardhini)," alisema Prof. Ndunguru.

Kuhusu ukusanyaji wa maduhuli ya serikali, katika mwaka wa fedha 2023/24 mamlaka iliazimia kukusanya Sh. 6,454,437,453 mapato ya ndani kwa kipindi cha miezi mitatu, Julai hadi Septemba, mwaka 2023.

Prof. Ndunguru alisema, mamlaka imekusanya Sh. 6,143,965, 337 sawa na asilimia 95.2 ya makadirio ya makusanyo ya mwaka mzima kutoka kwenye vyanzo vyake mbalimbali vya mapato ya ndani.

"Kwa kipindi cha mwezi Oktoba hadi Desemba 2023, mamlaka imekusanya Sh. 5,352,196,967 na kwa kipindi cha Januari 6 hadi Machi, mwaka huu, mamlaka imekusanya Sh. bilioni 3.7.

# Programu kuimarisha sekta ya elimu yazinduliwa

**Na Restuta James**

SERIKALI imezindua programu ya kuboresha kada ya ualimu inayolenga kuimarisha sekta ya elimu ikiwamo ajira, motisha, ufadhili wa mafunzo na ujenzi wa nyumba za walimu nchini.

Aidha, imetenga Sh. bilioni 215 kwa ajili ya maboresho hayo huku Mfuko wa Shirika la Ushirikiano wa Elimu Duniani (GPE), likitenga dola za Marekani milioni 80 kwa ajili ya Tanzania.

Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, alisema hayo jijini Dar es Salaam jana katika hafla ya uzinduzi wa programu hiyo inayotoa fursa ya elimu bora na jumuishi kwa wanafunzi na walimu wa shule za awali, msingi na sekondari.

Alitaja maeneo mengine ya msisitizo kuwa ni kuwezesha mfumo wa uandaaji ufundishaji jumuishi unaotumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), kujenga vituo vya mafunzo kwa walimu, kuwa na mfumo jumuishi wa upangaji wa walimu kwa njia ya elektroniki kwa kuzingatia jinsia, kununua vifaa vya usaidizi na kutoa ufadhili wa mafunzo kwa walimu wanaofundisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

"Ni lazima tuwekeze sana kwa walimu na niahidi hapa kwamba yale yanayotuhusu kwa ajili ya kada hii tutayashughulikia haraka ili walimu waweze wawahudumie watoto kule shuleni...kumekuwa na mtindo wa wasimamizi wa walimu kujumuisha taaluma ya ualimu pale inapotokea mwalimu mmoja anatenda kinyume cha maadili. Mwalimu mmoja anapokosea ashughulikiwe yeye mwenyewe taaluma ya ualimu iheshimiwe," alisema Dk. Biteko.

Alisema kwenye vituo vya mafunzo kwa walimu, serikali itafunga mifumo ya TEHAMA itakayowawezesha kupakua vitabu na mahitaji muhimu ya ufundishaji na pia itaruhusu walimu wa kujitolea kwenye maeneo yenye uhaba mkubwa wa walimu.

"Kazi ya kuboresha elimu ni ya kudumu, tunaomba wadau msituchoke...hili si jukumu la serikali peke yake, inahitaji juhudi za pamoja za wadau wote," alisema Dk. Biteko na kuyaomba mashirika ya kimataifa, kampuni na taasisi binafsi na asasi za kiraia kuunga mkono kazi hiyo.

Dk. Biteko alisema serikali imeendelea kuongeza bajeti ya elimu kwa asilimia 20.4 kutoka Sh. trilioni 4.7 mwaka 2021/22 hadi Sh. trilioni 5.7 mwaka 2023/24.

Alisema katika miaka mitatu ya Serikali ya Awamu ya Sita, walimu 37,473 wameajiriwa, 227,383 wamepandishwa madaraja na zaidi ya 20,000 wamepandishwa vyeo.

Alitaja changamoto zinazoikabili sekta ya elimu ni pamoja na upungufu wa walimu, madarasa, vitabu na nyumba za walimu, inayotokana na ongezeko la udahili wa wanafunzi kuanzia ngazi ya awali hadi kidato cha nne.

"Kwa mfano mwaka huu watoto waliodahiliwa kuingia shule ya msingi ni milioni 10.8 ambao wamefanya uhitaji wa madarasa ni 96,166 na ongezeko hili litakuwa kubwa zaidi mwaka 2030 ambapo udahili utakuwa ni zaidi ya milioni 12," alisema.

Ili kukabiliana na upungufu wa nyumba za walimu, alisema katika programu hiyo, mkazo unawekwa kujenga nyumba kwa walimu katika halmashauri za pembezoni.

Alimtaka Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, atoe zawadi kwa walimu wanaofanya vizuri ili kutambua mchango wao wakati wa maadhimisho ya Siku ya Walimu Duniani, ambayo huadhimishwa Oktoba 5, kila mwaka.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Shirika la Ushirikiano wa Elimu Duniani (GPE), Dk. Jakaya Kikwete, alisema GPE iliyoanzishwa na Nchi Saba Tajiri zaidi duniani (G7), inalenga kuimarisha maendeleo ya elimu katika nchi masikini na kwa sasa inahudumia nchi 89 ikiwamo Tanzania.

Alisema kupitia shirika hilo, Tanzania imepata ufadhili uliowezesha kuchapisha vitabu milioni 36, kuimarisha mifumo ya elimu, kujenga madarasa ya elimu ya awali 300, ya shule za msingi 2,980, vituo vya walimu 252, nyumba 64 za walimu, shule mpya 18 na mabweni ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu 15.

Alisema katika programu hiyo, Tanzania itapata dola za Marekani milioni 80.

Aliipongeza Tanzania kwa kuongeza udahili wa wanafunzi kwa ngazi zote na kuitaka serikali ifanye utafiti wa sababu za watoto wengi kukatisha masomo kabla ya kuhitimu.

"Takwimu zinaonesha watoto milioni 240 wako nje hawako darasani kati yao milioni 100 wako Afrika. Hili ni tatizo kubwa...wale wanaojiunga na shule, asilimia 33 hawamalizi," alisema.

Awali, Prof. Mkenda, alisema programu hiyo itatumia Sh. bilioni 212 na maeneo ya kipaumbele ni vitendea kazi, miundombinu, ubora wa walimu na wakufunzi, ajira na motisha kwa walimu.

Alisema serikali imeshafanya maboresho ya sera na sheria ili elimu ya lazima iwe ni awali mpaka kidato cha nne kwa maana ya miaka 10, kuwaongezea walimu ujuzi, huku wapya wakichujwa kwa mitihani maalumu kama inavyofanyika kwenye kada nyingine.

Balozi wa Sweden nchini, Charlotte Ozaki Maclas, alisema wadau wa maendeleo wako tayari kushirikiana na serikali katika programu hiyo kwa kuwa walimu ndio kichocheo cha maendeleo ya jamii.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo, Husna Sekiboko, alitaka serikali itumie kwa uaminifu fedha za wafadhili ili kutatua kero zilizopo kwenye sekta ya elimu na mkazo uwekwe kwenye kuajiri walimu na kuboresha maslahi yao.

HABARI KITAIFA

## Kiwango udumavu watoto chashuka

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Mstaafu wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, amesema kiwango cha hali ya udumavu kwa watoto walio chini ya miaka mitano kimeshuka nchini.

Amesema alipoingia madarakani hali ya udumavu kwa kundi hilo, ilikuwa ni asilimia 42 na alipotoka mamlakani mwaka 2015, kilifikia asilimia 34.

Kikwete aliyasema hayo jana jijini Dar es Saalam, wakati wa hafla ya makabidhiano ya vidonge milioni 22 vya Vitamin A kutoka Shirika la Nutrition International kwa Wizara ya Afya. Alisema kwamba hali ya udumavu nchini kwa sasa imefikia asilimia 30 kwa mujibu wa wizara hiyo huku akisema kiwango hicho bado ni kikubwa kutokana na udumavu kuwa miongoni mwa vyanzo vya vifo kwa kundi hilo.

"Udumavu ni pamoja na ukondefu, kimo kisichokwenda sambamba na umri, uzito mdogo na anaemia. Asilimia 30 tuliyo nayo bado ni kubwa. Nilipotika madarakani ilikuwa asilimia 34, tumejitahidi kushuka kwa asilimia nne," alisema Kikwete.

"Nilipostaafu Shirika lilinitaka niwe mjumbe wa bodi, nikaona nikubali kwa sababu haitaathiri shughuli zangu za kilimo, Msoga...tunamshukuru nchi ya Canada, kupitia shirika hili kwa msaada huu," aliongeza.

Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, alisema Tanzania kiwango cha watoto walio chini ya miaka mitano ni milioni 11, hivyo vidonge milioni 22 vitatolewa kwa awamu mbili, Juni na Desemba mwaka huu.

"Vidonge hutolewa katika siku 30 za mwezi Juni, na siku 31 za mwezi Desemba, hivyo ni awamu mbili. Vidonge hivi vitainua kiwango cha afya za watoto hawa.

"Tatizo jamii bado haijaelimika kuhusu lishe bora, wengi wanadhani ukishiba ndio lishe. Kushiba sio lishe, je, tumekula chakula gani ukashiba? Tuzingatie lishe ya mtoto, na wote pia," alisema.

# 10,000 hawajaripoti kidato cha I

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

ZADI ya wanafunzi 10,000 kati ya 56,827 waliochaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule za sekondari za serikali mkoani Morogoro mwaka huu, hawajaripoti na kusajiliwa hadi kufikia Februari 23.

Hayo yamebainishwa kwenye taarifa ya Ofisa Elimu Taaluma wa mkoa huo, Hildegard Saganda iliyowasilishwa wakati wa kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Morogoro (RCC).

Alisema hadi kufikia Februari 23, idadi ya wanafunzi walioripoti na kusajiliwa shuleni ilikuwa 46,775 sawa na asilimia 82. Kati yao, wavulana ni 22,203 na wasichana ni 24,572.

Alitaja halmashauri zenye wanafunzi wengi ni Kilosa ambayo waliochaguliwa ni 11,156 wakati walioripoti hadi kipindi hicho walikuwa 8,990 sawa na asilimia 81 ikifuatiwa na Manispaa ya Morogoro ambako waliochaguliwa ni 9,885 na walioripoti 7,502 sawa na asilimia 76.

Ofisa Elimu huyo alisema uandikishaji wanafunzi elimu ya awali na darasa la kwanza kwa mwaka 2024 umekuwa wenye mafanikio makubwa.

Alisema hadi kufikia Februari 23, mwaka huu, jumla ya wanafunzi wa awali 74,792 wakiwamo wavulana 37,786 na wasichana 37,006 wameandikishwa kati ya 93,551 sawa na asilimia 79.95 waliotarajiwa.

Pia alisema wanafunzi 86,408 wakiwamo wavulana 43,357 na wasichana 43,051 wameandikishwa kuanza darasa la kwanza kati ya 84,642 waliotarajiwa ambao ni sawa na asilimia 102.1.

Upande wa elimu ya awali, Ofisa Elimu alisema Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa imeongoza kwa kuandikisha wanafunzi 15,588 kutoka kwenye matokeo ya idadi ya 18,063, ikifuatwa na Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero kwa wanafunzi 10,427 kutoka kwenye maoteo ya 12,569.

Kwenye uandikishaji wa darasa la kwanza kati ya halmashauri tisa za mkoa huo, Kilosa imeongoza kwa kuandikisha wanafunzi 17,421 tofauti na maoteo yake ya wanafunzi 16,616, ikifuatwa na Mvomero iliyoandikisha wanafunzi 11,471 kutoka maoteo ya wanafunzi 11,871.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo ya RCC, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, aliagiza wakuu wa wilaya na wakurugenzi kuhakikisha wanasimamia kwa karibu suala la elimu katika maeneo yao.

Wajumbe wa RCC pia walipitisha makadirio ya Sh. bilioni 484.054 kwa ajili ya bajeti ya mkoa huo kwa mwaka wa fedha 2024/25.



Mtaalamu wa maabara wa Kituo cha Afya Kimara, Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam, Lizaline Bwakila (kulia), akimtoa damu, Maximilian Michael, katika zoezi la uchangiaji damu lililoendeshwa na Idara ya Vijana ya Kanisa la Waadventista Wasabato Mbezi Luis juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Kamati Bunge yageukia usimamizi mipango matumizi ardhi

**Na Munir Shemweta,**
RUANGWA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, imetaka mipango ya matumizi ya ardhi inayotekelezwa katika vijiji mbalimbali nchini kusimamiwa ipasavyo na kamati za vijiji ili kuleta tija.

Aidha, kamati hiyo imeipongeza Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa kutekeleza miradi ya mipango ya matumizi ya ardhi kupitia Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi katika vijiji mbalimbali nchini.

Kwa mwaka 2023/24 wizara kupitia Tume ya Taifa ya Matumizi ya Ardhi na wadau wengine, imetekeleza miradi ya mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji 333 nchini kote.

Mradi wa upangaji matumizi ya ardhi unatekelezwa na wizara kupitia tume hiyo ambayo imepewa jukumu kisheria la kuwezesha na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi katika ngazi mbalimbali nchini. Mipango hiyo huandaliwa katika ngazi ya taifa, kanda, mikoa, wilaya na vijiji.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi Maliasili na Utalii, Timotheo Mnzava, akiwa katika ziara ya kamati hiyo jana katika kijiji cha Namkatila wilayani hapa, alisema kupanga mipango ya matumizi ya ardhi ni jambo moja na kuisimamia na kutekeleza ni jambo lingine.

Alibainisha kuwa kazi ya kusimamia mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji si ya waziri, tume na wala wakuu wa wilaya ndiyo maana ziko kamati za vijiji zilizotokana na wananchi wa vijiji husika.

"Niombe mipango ya matumizi ya ardhi iliyotumia fedha za nchi na walipakodi kuitengeneza ikasimamiwe na kuheshimiwa na wenzetu katika kamati wasaidie ili mipango hiyo ikalete matokeo na matumda yaliyokusudiwa.

"Tukiwa na mipango tunajisifia tumeipanga halafu hatuifuati itakuwa ni kazi bure na huko vijijini wenyeviti na wenzao wakuendelea na ujanja ujanja wa kuuza maeneo bila kufuata mipango iliyopangwa, hatuwezi kutoka na haiwezi kutusaidia," alisema Mnzava.

Awali, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, alisema utekelezaji wa miradi ya upangaji matumizi bora ya ardhi katika vijiji mbalimbali nchini ni maono ya wizara kuona vijiji vyote vinakuwa katika mpangilio mzuri.

alisema kwa wilaya ya Ruangwa, tume imetekeleza mradi katika vijiji 16 vikiwamo Chikwale, Chihundu, Nambilanje, Mkaranga, Nanganga, Chikoko na Likwachi.

Kwa mujibu wa Pinda, tume imewezesha uandaaji mipango kina wa maeneo ya makazi kwenye kijiji cha Namkatila uliowezesha uandaaji wa hati za kimila 787 na upimaji mipaka ya vijiji 10 pamoja na upimaji mipaka ya vijiji uliowezesha utatuzi wa migogoro ya mipaka ya muda mrefu hususan mgogoro wa mpaka kati ya vijiji vya Nanjaru na Mnyangala vilivyopo katika Manispaa ya Lindi.

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii imefanya ziara ya kukagua utekelezaji wa mradi wa kupanga matumizi ya ardhi katika Halmashauri ya Wilaya ya Ruangwa.

Kamati pia ilikabidhi vyeti vya ardhi ya vijiji, ramani za mipaka iliyopimwa na kuhuishwa, mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji na Hati za Hatimiliki za kimila kwa wananchi.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Chanjo ya malaria itasaidia kudhibiti vifo

**HABARI** njema kutoka kwa wataalam wa Taasisi ya Afya Ifakara (IHI) ambao wako katika hatua ya mwisho ya utafiti wa chanjo nyingine ya malaria yenye uwezo wa kuzuia maambukizi ya ugonjwa huo kwa asilimia 75 inatia matumaini ya kudhibiti vifo vitokanavyo na ugonjwa huo.

Ugonjwa wa malaria ni hatari na usipowahiwa mapema kutibiwa husababisha vifo huku takwimu zikionesha kuwa ugonjwa huo unaua haraka kulinganisha na magonjwa mengine.

Chanjo husaidia kwa kiasi kikubwa kudhibiti mtu kupata ugonjwa na hata akiupata hauwezi kuleta madhara makubwa kama atakuwa hajapata chanjo.

Hilo limejidhihirisha pia wakati ugonjwa wa UVIKO-19 ulipoitikisa dunia na kusababisha maelfu ya watu kupoteza maisha.

Vifo vingi vilitokea kwasababu watu walikuwa hawajapata chanjo mapema ya kudhibiti ugonjwa huo na ilipopatikana matokeo yalionekana kutokana na madhara yake kupungua kwa kiasi kikubwa.

Chanjo za kudhibiti magonjwa mbalimbali hasa ya milipuko, zimesaidia kudhibiti magonjwa hayo kusambaa kwa kasi na kuleta athari kwa binadamu.

Kuna chanjo ya ugonjwa wa surua, polio, ndui ambazo kabla ya kupatikana kwake watu wengi waliathirika kwa kupata ulemavu wa kudumu au kusababisha vifo.

Ndio maana tunasema matokeo ya utafiti wa chanjo hiyo mpya ya malaria inasubiriwa kwa hamu kubwa ili kudhibiti ugonjwa huo hatari.

Kutokana na mbu kuwa sugu kwa baadhi ya dawa zinazotumika kuwaua, ugonjwa huo umekuwa ukiwatesa watu wengi na matibabu yake yamekuwa na gharama.

Hata katika baadhi ya hospitali mtu anapokwenda kuchukuliwa vipimo vya malaria, havioneshi kama ana vijidudu hivyo, na badala yake anaambiwa kuwa ana maambukizi katika njia ya mkojo.

Mtu anaweza kupoteza maisha kwa kutibu ugonjwa mwingine ambao haumwi na ule unaomsumbua ukiendelea kumshambulia.

Ugonjwa wa malaria kwa mujibu wa watalaamu husababisha damu nyingi kupotea na matokeo yake kuhitaji kuongezewa na kama atachelewa kifo kitamkabili.

Kwa mujibu wa wataalamu wa utafiti wa chanjo hiyo mpya ya malaria, chanjo ya kwanza ilikuwa na ubora kwa asilimia katia ya 36 na 40.

Lakini hii mpya inatarajiwa kuwa na uwezo wa kuzuia maambukizi ya ugonjwa huo kwa asilimia 75.

Chanjo hiyo iliyo katika utafiti kwa mujibu wa watalaamu imeonesha mafanikio makubwa, yenyewe ina ufanisi wa asilimia 75 na imelenga watoto zaidi ambao wako katika kundi hatarishi kwa wanao athirika zaidi.

Aidha, imeelezwa kuwa utafiti wa chanjo hiyo mpya (R21) uko kwenye hatua ya tatu na ya mwisho, lakini haijaingia sokoni.


Kwa Tanzania tunasema hayo ni mafanikio makubwa katika kudhibiti ugonjwa huo kuendelea kutesa wananchi na serikali kupunguza gharama ya kuagiza dawa za kuponya ugonjwa huo.

Kama Zanzibar waliweza kudhibiti ugonjwa huo na 'Zanzibar bila malaria' ikawezekana kupitia mradi wa malaria, hata kwa upande wa Bara inawezekana.

Cha msingi ni watu pia kuweka mazingira yanayowazunguka katika hali ya usafi na kuondoa vyanzo vyote vinavyosababisha mazalia ya mbu wanaoeneza ugonjwa huo.

Vile vile, ni muhimu kuzingatia kutumia chandarua kilichowekwa dawa wakati wa kulala ili wadudu hao wasiweze kupenya na kushambulia binadamu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Pilly Kigome

# Mwezi Mtukufu umeanza, tujifunze na kujirekebisha jamii ivutiwe nasi

**SIKU** ya Machi 12, waumini wa dini ya Kiislamu Tanzania na duniani kote kwa ujumla, wameanza kutekeleza ibada muhimu ya kutimiza Nguzo ya Nne katika Nguzo Tano, zinazosimamisha dini hiyo ambayo ni kufunga Mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Kwa mujibu wa maandiko ya dini ya Kiislamu, kuna nguzo tano ambazo ni msingi zinazosimamisha imani ya dini hiyo na kila muumini wa dini hiyo, anatakiwa atekeleze nguzo hizo, ndipo ahesabike kuwa ni miongoni mwa waumini wa dini hiyo.

Kati ya hizo tano, kuna moja ambayo si lazima muumini kuitekeleza japo ni muhimu kwa walioamini, kwa kuwa maandiko yanasema ni 'kwa wale wenye uwezo pekee wa kufanya hivyo.'

Nayo ni ile ya kwenda kuhiji Mji Mtakatifu wa Makka, kwenye nyumba tukufu. Maandiko yanasema, hii ni kwa wale wenye uwezo wa kifedha na afya, ni lazima wafanye hivyo, ili waweze kwenda kutekeleza ibada hiyo muhimu.

Ngoja nizitaje nguzo hizo tano muhimu kwa mtiririko maalum kwa mujibu wa maandiko kutoka katika Kitabu Tukufu cha Quruan.

Nguzo ya kwanza, ni kumuamini Mwenyezi Mungu na mjumbe wake Muhammad (SAW). Ya pili ni kuswali swala tano katika vipindi tofauti, vilivyopangwa katika mtiririko maalum pasipo kuuvuruga.

Nguzo ya tatu, ni kutoa zaka na ya nne, ni Kufunga Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na ya Tano, ni kwenda Kuhiji Mji Mkukufu kwa wale wenye uwezo.

Hebu naomba tukumbushane nikiwa ni mmoja wa muumini wa dini hiyo mwezi huu tunatakiwa tutende mambo yaliyo mema, kufanya mambo ya kheri na isiwe tufanye tu katika mwezi huu la hasha, bali iwe ni mwendelezo katika kuyaendeleza hayo mambo mema na mazuri.

Imekuwa na mazoea ya waumini hao kujisahau kwa kiwango kikubwa sana kwa kumuongopea Mungu dhahiri, shahiri kwa kipindi hiki kujifanya ama kujinasibu ni watu bora na kipindi hiki kiisha wanarudi na kufanya mambo ya hovyo.

Kwa pamoja, tukishirikiana kufanya mambo mazuri na safi basi naamini hakutakuwa na mambo ya uvunjifu wa amani nchini, hakutakuwa na ukatili wa kijinsia, hakutakuwa na aina yoyote ya wizi na nchi itabaki kuwa na amani na salama.

Ukweli ni kwamba, katika kipindi hiki cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani, ndicho kinachowakumbusha Waislamu walio wengi kufanya mambo mema na mazuri.

Kutokana na ukweli huo hata viongozi wa dini wa kiislamu kutoka maeneo tofauti tofauti wamekuwa wakitumia kipindi hiki katika kuwajenga waislamu kwani kumekuwa na wingi ama mafuriko wa waumini katika nyumba za ibada.

Hii inatokana na kujiangalia kwa matendo yao maovu hivyo wengi kuonekana kumrudia mungu na kubadilika kitabia.

Mufti Mkuu wa Tanzania, Abubakar Zuberi, wakati akiwatangazia waislamu kuanza kwa kutekeleza ibada hiyo aliwataka Waislamu kote nchini kuishi kwa upendo na amani na kuwataka wazidishe kuomba msamaha kwa Mwenyezi Mungu, pasi na kuiombea nchi iendelee kuwa na amani isiingie migogoro.

Aliwataka na kuwaomba waumini wa dini ya Kiislamu kuwaombea viongozi wetu wakuu wa nchi, ikiwamo na kuiombea nchi kuepukana na mabalaa na maradhi makubwa katika nchi yetu.

Mbali na dini ya Kiislamu, dini zote nchini zinahubiri amani, upendo, kusamehemana na kuomba sana Mungu, unyenyekevu kutendeana mema

Rai yangu mbali na kuutumia mwezi huu mtukufu wa Ramadhan vizuri mimi napenda kusema ndugu zangu Waislamu wenzangu tuendeleze mazuri yetu na mema yetu hata kama mwezi huu utaisha.

Nirudi kwa upande wa wazazi tunatakiwa tujitahidi katika malezi ya watoto yetu kwani kumekuwa na mmomonyoko wa maadili katika jamii yetu basi tuutumie vyema mwezi huu pia katika kujenga tabia zilizo njema kwa watoto wetu.

**Ramadani Mubaraqa!**

## Uwekezaji mdogo kikwazo malezi na makuzi ya watoto

**Na Sabato Kasika**

UTAFITI mbalimbali uliofanywa Afrika, umebaini uwekezaji kwa malezi na makuzi ya watoto wadogo, bado ni mdogo na hauna uwiano sawa kama unavyobainishwa na sayansi ya malezi ya watoto.

Waziri wa Mandeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, aliyemwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan, katika mkutano wa kimataifa wa malezi na makuzi maendeleo ya awali ya mtoto kwa nchi za ukanda wa Afrika Mashariki, unaoendelea Dar es Salaam, alibainisha matokeo hayo bila kufafanua kwa kina.

Dk. Gwajima alisema hali hiyo ikiendelea bila kuchukuliwa hatua zaidi, mataifa ya Afrika yatakuwa yanaandaa watoto, lakini hatimaye kuwa na nguvu kazi isiyo na tija kwa mataifa husika.

Alisema kuna haja kwa mataifa ya Afrika kuimarisha uwekezaji kwa watoto wadogo kwa kutumia mapato ya serikali zao na kushirikisha wadau wa maendeleo kusaidia katika eneo hilo la malezi.

"Serikali ya Tanzania imeandaa na inatekeleza Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto ya miaka mitano. Tanzania ni nchi kubwa, lakini kupitia serikali na wadau wa maendeleo; programu hii inatekelezwa nchi nzima," alisema.

Aidha, alisema katika kuonyesha utashi wa utekelezaji wa programu hiyo kwa mwaka ujao wa fedha 2024/25, serikali ya imeelekeza mikoa na halmashauri zote kutenga fedha katika bajeti zake ili kutekeleza afua za malezi na makuzi ya watoto.

"Katika kipindi cha miaka miwili ya utekelezaji wa programu hii tumefanikiwa kwa kiwango kikubwa, nimeambiwa kuwa mtaalamu kutoka Tanzania atawasilisha mada kuhusu uratibu na utekelezaji wa programu hiyo, hivyo atafafanua kwa kina kuhusu utekelezaji huo," alisema. Mkurugenzi wa Mtandao wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto Tanzania, Mwajuma Rwebangira, amesema kuna haja kwa wadau kuendelea kujitokeza kushirikiana na serikali, ili kutekeleza Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto na kuleta matokeo chanya katika jamii.

"Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto imelenga kuifikia jamii hasa wazazi, walezi na watoto kwani hatua hii itasadia kuwa na watoto watakaoleta mabadiliko na maendeleo katika jamii yao ya baadaye," alisema.

Madau wa masuala ya malezi na makuzi ya mtoto, Profesa Mary Getui kutoka Kenya, alisema elimu ya malezi na makuzi kwa mtoto ni ya muhimu na kwamba kila nchi Afrika haina budi kuchukua hatua kuhakikisha inakuwa na jamii bora.

"Ninaamini kila nchi ina changamoto zake katika malezi, hivyo kupitia mkutano huo tutapeana uzoefu, ili kusaidia katika malezi na makuzi ya watoto wetu," Prof. Getui alisema.

Mwakilishi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Tanzania, Dk. Charles Moses, alisema shirika hilo na wadau wengine wataendelea kuipa kipaumbele ajenda ya malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto kwa kuwa ni miongoni mwa mambo yanayoyapa uzito kwa zaidi ya miaka 40 sasa.

"Kwa sasa dunia inakadiriwa kuwa na watoto milioni 250, wengi wao ni wale wanaotoka katika nchi za kipato cha kati, wana uwezekano wa kuwa katika hatari ya kufikia ukuaji kamili," alisema Dk. Moses.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila alikemea mtindo wa baadhi ya watu kuwaita watoto waliopo mitaani kwa jina la 'watoto wa mitaani', kwa kuwa hakuna mtaa unaozaa watoto bali wanatoka katika familia zao kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo za malezi duni.

"Dar es Salaam inakisiwa kuwa na watu zaidi ya milioni tano, hivyo hata watoto watakuwa wengi. Wito wangu ni kwamba tuzingatie malezi bora ili wasiwapo wanaokimbilia mitaani na kuitwa watoto wa mitaani," alisema Chalamila.



Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JCKI), Dk. Peter Kisenge (kulia), akipokea zawadi ya kitabu kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Global Education Link (GEL), Abdulmalik Mollel, alipotembelea ofisi za Global Medicare, eneo la Chang'ombe, jijini Dar es Salaam jana, ambapo taasisi hizo zimekubaliana kushirikiana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Msajili ataka mapato kufikia asilimia 10

**Na Elizabeth Zaya**

MSAJILI wa Hazina, Nehemiah Mchechu, amesema Rais Samia Suluhu Hassan ameagiza taasisi zote za serikali kuongeza mapato yasiyo ya kikodi kutoka asilimia tatu ya sasa hadi asilimia 10 ndani ya miaka mitano.

Mchechu alisema hayo juzi wakati wa ufunguzi wa mkutano wa siku tatu unaofanyika mjini Kibaha mkoani Pwani baina ya ofisi hiyo ya msajili, taasisi pamoja na mashirika ambayo serikali ina hisa chini ya asilimia 50.

"Rais ametaka kuwe na ongezeko kubwa la mapato yasiyo ya kikodi kutoka katika ngazi zote za serikali, kwa sasa mapato yasiyo ya kikodi ni asilimia tatu (3), anataka asilimia hii ifikie 10 ndani ya miaka mitano.

Tunaamini tutafikisha kwa sababu tumejipanga, tunaenda vizuri chini ya wizara ya mbili ambazo zinasimamia kwa kina za Mipango na Uwekezaji pamoja na Wizara ya Fedha, kwa kushirikiana na wizara zote ambazo taasisi hizo zimewekezwa ili kusimamiwa kisera kwa shughuli za kila siku," alisema. Alisema ofisi hiyo ina nafasi kubwa ya kusimamia mapato hayo yasiyo ya kikodi.

"Unapozungumzia mapato ya nchi, yamegawanyika katika sehemu kuu mbili, yaani mapato ya kodi na yasiyo ya kikodi. Na sisi Ofisi ya Msajili tuna nafasi kubwa ya kusimamia mapato yasiyo ya kikodi kwa sababu yale ni magawio na faida zinazotoka kwenye mashirika ya umma na uwekezaji wa serikali," alisema Mchechu.

Alisema ofisi yake imejipanga kufanikisha agizo hilo la Rais Samia la kukuza mapato yasiyo ya kikodi kutoka katika ngazi zote za uwekezaji wa serikali.

Akifungua mkutano huo, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dk. Natu Mwamba, alizitaka taasisi na mashirika hayo yenye hisa na serikali, kutambua na kuelewa kwamba jukumu lao ni kuangalia na kulinda maslahi ya nchi, ili serikali ipate gawiwo la kutosha na kutunisha mfuko wa serikali kuiwezesha kutekeleza maendeleo na ustawi wa jamii.

Dk. Mwamba alisema taasisi hizo za serikali zinapaswa kuchangia na kuwa gurudumu la maendeleo katika nchi kwa kutambua maeneo muhimu ya kuyawekea nguvu.

"Tunataka zihakikishe zinaongeza mfuko mkuu wa serikali ili kufanya mambo mengine ya kijamii na kimaendeleo inayopaswa kufanya. Kwa hiyo viongozi hawa wanapaswa kujua kwamba jukumu kubwa wanalopaswa kufanya ni kuangalia na kulinda masilahi ya nchi yetu ili tupate gawiwo la kutosha na kuongeza mfuko mkuu wa serikali.

"Kwa hiyo ni muhimu wakurugenzi za taasisi hizi, kuelewa picha kubwa ya namna mashirika ya umma yanavyopaswa kuendeshwa chini ya ofisi ya msajili wa hazina na majukumu wanayopaswa kuyatanguliza," alisema.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Walia na kiwanda kutiririsha maji machafu katika makazi

**Na Julieth Mkireri**, KIBAHA

WAKAZI wa Mtaa wa Lulanzi, Kata ya Picha ya Ndege, Halmashauri ya Mji wa Kibaha wamemwomba Mkuu wa Wilaya ya Kibaha kutatua kero ya maji machafu yanayotiririka toka kiwanda cha Keds.

Wananchi hao wamesema mbali ya maji hayo kuwa kero kwenye makazi yao, pia yanaweka rehani usalama wa mifugo inayokunywa maji hayo, pia kitoweo kitokanacho na mifugo hiyo.

Kiwanda hicho kinajihusisha na utengenezaji taulo za watoto na sabuni za unga ambazo zinasambazwa katika maeneo mbalimbali nchini. Kinalalamikiwa na wakazi jirani kutiririsha maji machafu ambayo yanakwenda kwenye makazi ya watu.

Kero hiyo iliibuliwa juzi wakati wa mkutano wa kusikiliza kero uliofanyika Picha ya Ndege, ukiandaliwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani.

Akizungumza katika mkutano huo, mmoja wananchi hao, Ramadhan Kalangaza alisema malalamiko yao yameshafikishwa kwenye mamlaka husika, lakini kero hiyo haijapatiwa ufumbuzi.

"Wananchi tumelalamikia kuwapo kwa kero ya maji machafu katika eneo la Lulanzi, tunaomba serikali kusaidia kutafuta ufumbuzi.

"Eneo hili pia kero ya kutopata maji safi na salama. Tunaomba suala hili lipatiwe ufumbuzi ili tufanye shughuli nyingine za maendeleo badala ya kuhangaika kusaka maji," aliwasilisha kero za wananchi wa eneo hilo.

Akitolea ufafanuzi wa kero hizo kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, Mkuu wa Wilaya ya Kibaha, Nickson Simon alisema kero ya maji machafu wanaifanyia kazi, wakianza kwa kukutana na uongozi wa kiwanda hicho.

Kuhusu kero ya wananchi kutopata huduma ya maji, Meneja wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira Dar es Salam (DAWASA), Alfa Ambokile alisema Mradi wa Maji Pangani ambao unatarajiwa kuanza hivi karibuni, utatatua kero hiyo katika eneo la Lulanzi na Kata ya Pangani.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha Dk. Peter Nsanya, akizungumzia kero za Hospitali ya Wilaya (Lulanzi0 alisema kuna jengo linajengwa katika hospitali hiyo kwa ajili ya kutatua kero ya ukosefu wa jengo la kuhifadhi maiti.

Dk. Nsanya alisema katika halmashauri hiyo hakuna jengo la kuhifadhi maiti na kwa sasa wanatumia lililoko Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Pwani (Tumbi).

Katika hatua nyingine, wakazi wa Kitongoji cha Kisabi, Halmashauri ya Wilaya ya Kibaha wameomba serikali kuridhia kuendelea kuishi katika kitongoji hicho kwa kuwa ndio eneo pekee wanalofanya shughuli zao za kilimo zinazoendesha maisha yao.

Wananchi hao zaidi ya 90 wamepatiwa eneo mbadala huko Kikongo kutokana na eneo wanakoishi sasa kutokuwa rafiki kwa ujenzi wa nyumba imara.

Serikali imetenga eneo lenye ukubwa wa ekari 1000 kwa ajili ya kuhamishia huko wananchi hao, lakini wamekataa wakilalamikia umbali wa kufikia maeneo yao ya kilimo ya sasa.

Mkuu wa Wilaya alichukua maoni hayo, akiahidi kuyafikisha kwenye ngazi husika kwa ajili ya kujadiliwa zaidi, akibainisha kuwa watakaohusika na maeneo yatakayotengwa ni wananchi 91 wanaotambuliwa na siyo 300 waliotajwa wakati wa mkutano huo.



Ofisa Fedha kutoka GGML, Joscar Rumanyika, akifafanua faida za programu ya ushauri kwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Kalangalala, mkoani Geita hivi karibuni. GGML imezindua programu hiyo, iliyopewa jina la 'GGML Ladies Mentorship Program' ikiwa ni sehemu ya wanawake wa kampuni hiyo kuadhimisha Siku ya Kimataifa ya Wanawake. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mfumo utoaji mikopo HESLB waimarishwa kuongeza tija

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imekamilisha kuunganisha mfumo wake mkuu wa kibenki na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) ili kuimarisha utoaji mikopo kwa wanafunzi.

Hatua hiyo inalenga kuwezesha wanafunzi kupata bidhaa za kibenki zenye ubora wa hali ya juu, ubunifu, usalama na ufanisi.

Akizungumza wakati wa kongamano lililofanyika jijini Dar es Salaam jana, likiandaliwa na HESLB na kuwakutanisha wadau mbalimbali wa elimu nchini, Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi wa Benki ya NMB, Filbert Mponzi, alisema mfumo huo kwa kiwango kikubwa umerahisisha utoaji mikopo kwa wanafunzi wa vyuo vikuu.

"Wanafunzi sasa watafurahia huduma za kibenki bila matatizo baada ya kuunganishwa kwa mfumo mkuu wa benki ya NMB na Bodi ya Mikopo. Sasa mikopo inatolewa kwa wanafunzi kwa haraka na kwa urahisi zaidi," Mponzi alisema.

Aliwataka wanafunzi wanufaika wa mikopo hiyo kufungua akaunti katika benki hiyo ili kunufaika na faida, ikiwamo mikopo ya papo kwa papo yenye masharti nafuu kuanzia Sh. 1,000 hadi 500,000. Mponzi alisisitiza dhamira ya benki hiyo kuendelea kufanya kazi kwa karibu na serikali pamoja na taasisi za elimu nchini ili kusaidia maendeleo ya sekta ya elimu kuanzia ngazi ya chini.

"Sekta ya elimu ni miongoni mwa vipaumbele vyetu muhimu. Ili kusisitiza dhamira yetu ya kusaidia elimu ya juu, mwaka jana tulitenga mikopo ya Sh. bilioni 200 kwa wanafunzi wa vyuo vikuu kufuatia majadiliano ya karibu na Wizara ya Elimu, Sayansi na Tekonlojia.

"Wanafunzi wanaweza kuomba mikopo kuanzia Sh. 200,000 hadi hadi Sh. milioni 10 kwa riba nafuu ya asilimia tisa tu,"

Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Dk. Bill Kiwia alisema lengo la kongamano hilo ni kupokea maoni toka kwa wadau mbalimbali wanaohusika na utendaji wa utoaji wa fedha kwa taasisi yake. Alisema bodi kwa sasa inawafikia zaidi ya wanafunzi 200,000 wenye uhitaji na imepanga kuwafikia wanafunzi wengi zaidi, lakini hilo litategemea upatikanaji rasilimali fedha.

"Hatujaridhishwa na hali ya sasa kwa sababu mahitaji ni makubwa kuliko rasilimali zilizopo. Bado tunatafuta rasilimali fedha mbadala ili kuwafikia wanafunzi wengi zaidi," alisisitiza.

Aliwataka wanufaika wa mikopo ya bodi yake kuhakikisha wanarejesha mikopo yao kwa wakati ili kuiwezesha taasisi yake kujiendesha kwa ufanisi kwa manufaa ya wanafunzi wengi wenye uhitaji.

## Mkurugenzi Jatu, DPP kuingia makubaliano

**Na Grace Gurisha**

ALIYEKUWA Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Jatu Public Limited, Peter Gasaya, anayetuhumiwa kutakatisha fedha za upatu, ameeleza mahakama nia yake ya kuingia makubaliano ya kukiri kosa na Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) baada ya kusota mahabusu gerezani kwa zaidi ya miaka miwili.

Taarifa hiyo ilitolewa jana na mshtakiwa kupitia wakili wake, Kung'he Wabeya mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Richard Kabate wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam kesi ilipoitwa kwa ajili ya kutajwa.

"Tayari tumeshaandika barua ya maombi hayo na tutawasilisha nakala ya barua hiyo kwa upande wa mashtaka leo (jana)," alidai Wakili Wabeya.

Wakili wa Serikali, Eva Kassa aliomba mahakama ipange tarehe nyingine ya kutajwa kesi hiyo kwa kuwa hawajakamilisha upelelezi wa shauri hilo.

Hakimu alikubali ombi hilo na kuwapa siku 30 pande zote mbili kufanya makubaliano hayo kisha waarifu mahakama hatua watakayofikia. Kesi hiyo iliahirishwa hadi Machi 26, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa.

Inadaiwa kuwa kati ya Januari Mosi, 2020 na Desemba 31, 2021, jijini Dar es Salaam, mshtakiwa akiwa kama Mkurugenzi wa kampuni hiyo, alijipatia Sh. 5,139,865,733 (Bil. 5.139/-) kutoka Saccos ya Jatu kwa njia ya udanganyifu.

Inadaiwa alijipatia kiasi hicho cha fedha kwa madai kwamba angezizalisha kwa kuwekeza katika mazao ya kilimo na kupata faida zaidi, jambo ambalo alijua si kweli.

Katika shtaka la pili, inadaiwa kwamba, Gasaya alitakatisha fedha hizo zilizokuwa katika akaunti ya Jatu iliyoko benki ya NMB Tawi la Temeke kwa kujihusisha katika miamala.

Inadaiwa mshtakiwa alifanya hivyo huku akijua fedha hizo ni mazalia ya kosa tangulizi la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

**Wakili wa Serikali, Eva Kassa aliomba mahakama ipange tarehe nyingine ya kutajwa kesi hiyo kwa kuwa hawajakamilisha upelelezi wa shauri hilo.**



## Loiborsoit kunufaika mpango wa bajeti 2024/25

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

WANANCHI wa Kata ya Loiborsoit wilayani Simanjiro mkoani Manyara, watanufaika na mpango wa bajeti ya mwaka wa fedha wa 2024/2025 uliopitishwa na Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, kupitia miradi mbalimbali kwa kugusa maisha yao.

Diwani wa Kata ya Siria, Baraka Kiduya, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema wananchi wa vijiji viwili vya kata hiyo, Loiborsoit na Ngage watanufaika kupitia miradi ya maendeleo.

Katika hatua nyingine ameishukuru serikali kwa namna inavyotekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwenye sekta ya elimu, afya, maji na barabara.

Alisema kupitia bajeti hiyo Kata ya Loiborsoit itanufaika kupitia miradi mbalimbali ya maendeleo.

"Katika mpango wa bajeti wa mwaka wa fedha wa 2024/2025 tumepata madarasa mawili ya shule shikizi ya Songoyo, Sekondari ya Loiborsoit tumepata mradi wa UVIKO na pochi ya mama," alisema diwani huyo.

Pia alisema kwa sekta ya afya serikali imefanikisha ujenzi wa zahanati mbili zilizoko kwenye kata hiyo, pia zitapatiwa miradi ili ziweze kuendelea kutoa huduma kwa jamii.

Amepongeza Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini(TARURA), kwa kujenga daraja linalounganisha wilaya ya Simanjiro na Same mkoani Kilimanjaro, lililoko kwenye kata hiyo.

Alisema mradi mkubwa wa maji wa Mto Pangani utawanufaisha wananchi wa kata kwa kuwa Shilingi bilioni 42 zimetengwa kutekeleza mradi na utakuwa mkombozi kwa wakazi wa vijiji vya Ngage na Loiborsoit na Ngarash.

# Mirerani kulindwa kila kitongoji kudhibiti uhalifu

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

JESHI la Polisi limewapanga askari watano kwa kila kitongoji cha mji mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro mkoani Manyara kudhibiti uhalifu.

Mkuu wa Kituo cha Polisi Mirerani, Mrakibu wa Polisi (SP) Dominick Fwaja, alisema hayo wakati akizungumza kwenye mkutano wa hadhara wa Mkuu wa wilaya hiyo, Dk. Suleiman Serera.

Mkutano huo, ulikuwa na dhamira ya kutembelea kitongoji kwa kitongoji na kusikiliza kero na changamoto zinazowakabili wananchi katika Kata ya Endiamtu, wilayani humo.

Alisema pia wamedhamiria kuwaonyesha wananchi dhana ya polisi jamii na ulinzi shirikishi inavyopatiwa ufumbuzi na kupunguza uhalifu.

Aidha, alisema katika vitongoji 24 vilivyoko katika mji huo, amewapanga askari polisi wanne mpaka watano kwa kila kitongoji ili waweze kufanya kazi ya kulinda raia na mali zao kwa ukaribu zaidi.

Alisema katika mpango wa kuhakikisha changamoto ya wizi, matukio ya uhalifu na vurugu zinamalizika wamekaa kikao na wenyeviti wa vitongoji na kuwapatia askari polisi hao ambao watakuwa wanahusika kwenye vitongoji hivyo.

"Polisi wote wameshakutana na wenyeviti wa vitongoji na kutoa namba zao za simu hivyo wakiwa wanawahitaji watawasiliana mara moja ili kukomesha matukio ya uhalifu," alisema Fwaja.

Hata hivyo, alisema lengo ni kuhakikisha askari polisi hao, wanashirikiana na wenyeviti wa vitongoji na wakazi wa maeneo husika kukomesha matukio ya uhalifu.

"Kwa ushirikiano wao watamaliza mambo yote madogo yaliyopo kwenye uwezo wao na makubwa yatakayowazidi watayaleta kituoni tushughulike nayo," alisema OCS Fwaja.

Mwenyekiti wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani, Adam Kobelo, alimpongeza Fwaja kwa kutekeleza majukumu hayo ya kuwapangia askari polisi hadi ngazi ya vitongoji.

"Kupitia askari polisi waliopangwa kwenye vitongoji, ninatarajia wenyeviti na wakazi wa maeneo husika watawapa ushirikiano wa kutosha katika kupiga vita uhalifu," alisema Kobelo.

Mwenyekiti wa Kitongoji cha TANESCO, Justin Abraham, alisema hatua hiyo ni nzuri kwa kuwa hivi sasa uhalifu umepungua kwenye eneo lake.

"Wezi wanaokuja kuiba hapa mtaani kwetu Tanesco sio wakazi husika wa huku wanatoka maeneo mengine kuiba hata kuku, hivyo kupitia askari hawa na kamati yangu ya usalama tumekomesha wezi," alisema.




Mbunge wa Muheza, mkoani Tanga, Hamisi Mwinjuma (kulia), akizungumza na mfadhili kutoka Taasisi ya uchimbaji visima ya Moo Maji Well Drilling Ltd, Mohammed Ainahdi katika Kijiji cha Mtindiro hivi karibuni, ambapo taasisi hiyo imetoa msaada wa kuchimba visima virefu vya majisafi na salama takribani 83 kwa ajili ya wananchi wilayani humo, ili kumtua ndoo mama kichwani. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# CAMARTEC mkombozi kilimo, soko la uhakika

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MWENYEKITI wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Deodatus Mwanyika, amesema Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini (CAMARTEC), ni mkombozi kwa wakulima na wafugaji kwa kuwa kimewasaidia kurahisisha na kuboresha shughuli ikiwamo kupata masoko ya uhakika.

Akizungumza jana jijini hapa, wakati wa kamati hiyo ilipotembelea kituo hicho, Mwanyika alisema kazi inayofanywa na kituo inapaswa kupongezwa kwa kuwa itawasaidia wakulima kwa zaidi ya asilimia 86.

"Nawapongeza sana kwa kuwa mmejikita katika utafiti na kutengeneza zana mbalimbali za kilimo na mifugo, mnaleta suluhisho kwa wakulima wa kawaida na wafugaji," alisema.

Aidha, alisema katika kituo hicho, kuna kila aina ya mashine zikiwamo trekta zenye uwezo wa kulima, kupanda na kuweka mbolea.

"Hakika huu ni ukombozi kwa wakulima wetu na zipo zingine za kuvuna michikichi na za kusaga nafaka na vyakula vya mifugo," alisema.

Hata hivyo, alisema kabla ya kuondoka mkoani Arusha, watachukua changamoto zao ili waishauri serikali kuzitatua kwa ajili ya kuwasaidia wakulima kwa kuwatengenezea mashine zinazoendana na mahitaji yao.


Kwa mujibu wa Mwanyika, mashine zilizotengenezwa nchini, zitasadidia kuachana na uagizaji wa mashine kutoka nje ya nchi kutokana na utengenezaji unaoendana na jiografia ya nchini.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, alisema serikali itaiwezesha CAMARTEC inakuza kilimo cha ufanisi na kuondoa changamoto ya kupoteza chakula baada ya kuvuna kwa kutumia mashine hizo.

"Hapa kuna mashine za kuchakata mabua na kuhifadhi kwa muda mrefu inamsaidia mfugaji wakati wa uhaba wa chakula na hakuna kinachopotea, hali hii itawezesha mifugo kuwa bora na yenye tija wakati wote," alisema.

Dk. Kijaji alisema wanufaika wakubwa wa utengenezaji mashine hizo ni vijana wote waliomaliza vyuo vya kati na vingine kupata ajira.

Mjumbe wa kamati hiyo, Yustina Rahi, alisema licha ya ubunifu na kazi nzuri inayofanywa na kituo hicho, kuna haja kuishauri serikali kuweka ruzuku kwenye mashine hizo ili kuwawezesha wakulima kumudu ununuzi wa mashine.





# CHADEMA yamkana Matiko kuwania ubunge wa Tarime

**Na Timothy Itembe,** MARA

SIKU chache baada ya Mbunge wa Viti Maalum, Esther Matiko kutangaza kuwania ubunge wa Tarime Mjini katika Uchaguzi Mkuu ujao, uongozi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Mkoa wa Mara umesema haumtambui kama mwanachama wao.

Kwa kutomtambua kama mwanachama wao, uongozi huo umesema hauwezi kumsimamisha Matiko kuwania ubunge kupitia chama hicho.

Hivi karibuni, Matiko alizungumza na waandishi wa habari nyumbani kwake na kutangaza nia ya kugombea ubunge kwa tiketi ya CHADEMA katika Uchaguzi Mkuu wa mwakani ili kuendelea kutumikia wananchi jimboni humo.

"Nimekuwa ninapokea wito kutoka kwa wachungaji na kada mbalimbali; kinamama, vijana, wafanyabiashara na watumishi wa umma wakiniomba nigombee.

"Muda ukifika nitagombea kama ilivyokuwa uchaguzi wa mwaka 2015. Jamii iliniomba kugombea nikafanya hivyo.

"Nikipata wito toka moyoni nitagombea kupitia chama changu cha CHADEMA katika Uchaguzi Mkuu wa 2025 ili kutumikia wananchi kama vile Mama (Rais Samia Suluhu Hassan) alivyojielekeza katika kutekeleza miradi mingi ya kijamii nchini," alisema.

Matiko alisema kuwa katika kipindi chake akiwa mbunge, alimaliza mgogoro kati ya wananchi wa Bugosi na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na kusaidia wananchi kulipwa na kupisha eneo hilo pamoja na mambo mengine mengi, hivyo akirejea kwenye nafasi hiyo atafanya mambo mengi zaidi.

Alipoulizwa na mwandishi wa habari hizi kuhusu kusudio hilo la Matiko ambaye ni miongoni mwa wabunge 19 wa viti maalum ambao wamekuwa katika mgogoro wa kimaadili na chama hicho, Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alisema tayari chama hicho kimetoa miongozo dhidi ya wabunge hao. Mnyika alisema miongozo hiyo imetolewa kuanzia ngazi za jimbo hadi mikoa yao, hivyo ni vyema uulizwe uongozi wa ngazi husika.

Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Mara, Lucas Ngoto, alisema chama hakimtambui Matiko kama mwanachama wao, na kama anataka kurejea CHADEMA, afuate taratibu za kuomba kuwa mwanachama.

Kuhusu kutia nia kugombea ubunge wa Tarime Mjini, Ngoto alisema kuna mwanachama mmoja tu aliyetangaza nia kwa jimbo hilo ambaye ni Bobu Chacha Wangwe. CHADEMA haina baraka kwa Matiko kugombea ubunge kwa tiketi ya chama hicho kwa sasa.

Alifafanua kuwa hata kama Matiko ataomba tena kuwa mwanachama wa CHADEMA, kupitishwa kuwa mgombea ubunge kwa tiketi ya chama hicho ni ngumu kwa kuwa kwa mujibu wa sheria tayari ameshachelewa.

"Kwa sasa yeye (Matiko) siyo mwanachama wetu, sijajua ni lini ataomba kujiunga na chama pamoja na kufanya mchakato wa kutia nia katika jimbo ambalo tayari lina mtiania na pia vikao vikafanyika kwa ajili ya kujadili na kupitisha.

"Huenda ana hatua zingine ambazo yeye (Matiko) anafahamu. Pengine ana chama kingine atakakogombea, anajua mwenyewe, lakini siyo CHADEMA," alisema Ngoto.

Matiko na wabunge wengine 18 wamekuwa na mgogoro wa kimaadili na CHADEMA, hata kufikia hatua ya kufutwa uanachama wa chama hicho.



Mkuu wa Mkoa wa Mara, Said Mtanda (kulia), akiwa na Kamati yake ya Ulinzi na Usalama, wakimpokea Katibu Tawala mpya wa mkoa huo, Gerald Kusaya, juzi ambaye amehamishiwa mkoani humo akitokea Mkoa wa Rukwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mama adaiwa kumuua mwanawe kisha kumla

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

NYANSOROLI Paul (38), mkazi wa Kijiji cha Mishepo, wilayani Shinyanga, mkoani hapa anadaiwa kuua mtoto wake, Nazael Kidia mwenye umri wa mwaka mmoja na miezi saba kisha kuanza kumla nyama.

Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Janeth Magomi, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa tukio hilo lilitokea Januari 4, mwaka huu.

Alisema mwanamke huyo, siku ya tukio aliondoka na mwanawe huyo kwenda kusikojulikana, lakini siku nne baadaye alirejea nyumbani akiwa hana mtoto na ndugu zake walipohoji, alidai amemla nyama.

"Jeshi la Polisi tulifika eneo la tukio na kuanza uchunguzi na mwanamke huyo alipohojiwa na askari, alisema amemuua mtoto wake kisha kula nyama yake kwenye mbuga yenye mashamba," alisema.

Kamanda huyo aliendelea kueleza kuwa timu ya Askari polisi pamoja na Jeshi la Jadi (Sungusungu) waliambatana na mama huyo huyo hadi kwenye mashamba alikodai kutekeleza tukio hilo.

Alisema kuwa baada ya kufika katika eneo hilo, walikuta fuvu la mtoto huyo, hivyo kumkamata mama huyo kwa ajili ya hatua za kisheria kutokana na tuhuma za mauaji ya mtoto wake.

Alisema jeshi hilo kwa kushirikiana na Mkemia Mkuu wa Serikali wanaendelea na uchunguzi wa tukio hilo ikiwa ni pamoja na kufanya vipimo vya vinasaba (DNA) ili kubaini uhusiano wa fuvu hilo na mama hiyo.

"Kwa sasa mama huyo yuko nje kwa dhamana lakini katika upelelezi wetu fuvu la kichwa cha mtoto huyo limechukuliwa sampuli kupima vinasaba ili kubaini kama mtoto ni wake kweli ndipo hatua zaidi za kisheria zifuatwe," alisema Magomi.

Hata hivyo, Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA) hairuhusu mtuhumiwa wa kosa linalohusiana na adhabu ya kifo kuachiwa na polisi kabla ya kufikishwa mahakamani.

# Wananchi wachanga milioni 16/- kujenga madarasa, vyoo

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WANANCHI wa Kata ya Mhongolo, Manispaa ya Kahama, mkoani Shinyanga wamechangishana fedha kila kaya na kupata Sh. milioni 16 zilizotumika kuanzisha ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa, ofisi moja ya walimu na matundu tisa ya vyoo katika shule za msingi na sekondari zilizoko eneo hilo.

Mwenyekiti wa Mtaa huo, Emmanuel Nangale, alibainisha haya jana alipozungumza na Nipashe kuhusu ushirikishwaji wananchi katika utekelezaji miradi ya maendeleo, hasa ya sekta ya elimu.

Alisema kuwa mwaka wa fedha 2023/24, wameshiriki kwa kuchanga kiasi hicho cha fedha ambacho kimesaidia kufikisha ujenzi huo hatua ya boma, wakisubiria serikali kukamilisha mradi.

Nangale alisema kuwa katika Shule ya Msingi Bomani wameanzisha ujenzi wa vyumba vinne vya madarasa na ofisi moja ya walimu.

Kwa Sekondari ya Nyashimbi, Nangale alisema wameanzisha ujenzi wa matundu tisa ya vyoo vya wanafunzi ili wawe na mazingira rafiki ya kujifunzia na kutimiza ndoto zao kielimu.

Mbali na miradi hiyo, alisema wananchi pia wameshiriki kikamilifu katika upandaji miti 2,000 katika Shule ya Msingi Bomani kwa lengo la kutunza mazingira.

Mkazi wa kata hiyo, Abdallah Suleiman, alisema wamekuwa wanashirikishwa katika shughuli mbalimbali za maendeleo na hivi karibuni walishirikishwa kwenye ujenzi wa mitaro ya maji na kila mwananchi alichangia fedha kuwezesha ujenzi huo na maji kwa sasa hayaingii ndani ya makazi yao kama ilivyokuwa awali.

Ibara ya 8(1)(d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977) inaelekeza wananchi kushiriki katika shughuli za serikali yao.

ama
ALHAMISI MACHI 14, 2024
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 12

**Tembo 400 wavamia vijiji na kuua wakisimamisha kilimo miaka mitatu**



Ukurasa 13

NEMC yawakusanya wachimba dhahabu wadogo, wawapa darasa la kuacha zebaki



Ukurasa 14

**Kituo Afya Chanika chamkosha Ummy, mbioni kupandishwa hadhi ya hospitali**

# Hatua zake Rais, kila ngazi kapigania mazingira, leo kateuliwa hadhi dunia

• Daima haijakosekana katika mikakati yake

**Na Mwandishi Wetu**

INAPOFIKIWA leo katika sekta ya mazingira, inabeba sura katika safari yenye mizi mrefu ubia wake, tangu akiwa Makamu wa Rais, Dk. Samia Suluhu Hassan.

Marejeo mojawapo ni katika kilele cha Siku ya Mazingira Duniani huko Butiama mkoani Mara mwaka 2017, Samia aling'aka kutaka kuchukuliwa hatua kali dhidi ya waharibifu wa mazingira.

Hapo Makamu wa Rais nchini Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, alikuwa anawahutubia wananchi katika kilele cha Siku ya Mazingira Duniani, kijijini Butiama, mkoani Mara akiwa na maelezo ya kina.

Ni katika hatua hiyo, akaagiza kuchukuliwa hatua kali kisheria kwa viwanda na migodi inayofanya shughuli za uzalishaji kwa kuharibu mazingira, ikiwamo utitirishaji kemikali

Baadaye miaka minne akiwa Rais, akaziagiza wizara tano kisekta nchini, zinazojumuishwa na: Kilimo, Uvuvi, Maji Mazingira na Ufugaji kuketi na kutumia nafasi zitokanazo na Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere.

Hapo akasisitiza uhifadhi wa mazingira katika vyanzo vya maji vinavyoujaza Mto Rufiji, kutokana na umuhimu wa mto huo katika Mradi wa Bwawa la Mwalimu Nyerere, mbaoa sasa unamkomboa Mtanzania kwa umeme, pia ndani yake kuna amani aya mazingira .

"Mkapime, maeneo hayo na myaweke katika mashamba makubwa kwa ajili ya kufanya mnada wa wazi kwa wawekezaji wa uhakika katika kilimo.

"Nawasihi pia mtenge maeneo maalum kwa ajili ya wakulima wadogo hasa wa maeneo hayo yatakayokuwa na Miundombinu ya umwagiliaji maji," anasema Rais Samia

Aidha, Rais Dk. Samia akaiagiza Wizara ya Mazingira ambayo kabla ya kuwa rais ilikuwa chini yake, aliitaka kuchukua hatua dhidi ya waharibifu wa mazingira katika vyanzo vya maji, mito na maeneo muhimu yanayotumika kama chanzo cha maji katika Bwawa la Mwalimu Nyerere

"Bwawa hili katika nyanja zote yanawezekana tu kama tutatunza mazingira katika vyanzo vya mabonde ya mito inayoleta maji mabwawani. Hapa nataka nisisitize umuhimu wa kutunza mazingira.

"Mradi tumeujenga kwa gharama kubwa na kwa kujinyima vitu vingi muhimu. Itakuwa ni dhambi kubwa kama hautatimiza malengo yake, kwa sababu ya uzembe na ubinafsi wetu.

"Kwahiyo, kulinda mazingira na kulinda mradi huu sasa ni suala la kufa na kupona," akatamka Rais Dk. Samia.

Zao la ufanisi wake katika kulinda na kutetea mazingira duniani, haikushangaza Septemba mwaka jana, Rais Dk. Samia, akateuliwa kuwa Mjumbe wa Bodi ya Ushauri ya Kituo cha Dunia cha Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi Duniani, ikiikweza Tanzania kimataifa.

Sasa ni hatua inayopongezwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo. akimtaja Rais Dk. Samia kuwa mfano katika usimamizi wa mazingira, hususan kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Dk. Jafo anasema kuwa hilo limejipambanua kwa kutekeleza miradi kimkakati, ambayo ni chachu katika hifadhi ya mazingira.

Anatoa mfano wa ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) ambayo itatumia umeme na zaidi ya shilingi trilioni 23 kwa mradi huo, ikiwa na mchango wa kupunguza gesi joto inayotafsiri mabadiliko ya tabianchi.

Mradi mwingine anautaja ni wa Mabasi wa Mwendokasi mjini Dar es Salaam, ambao sasa umeaminika na Tanzania kuwa mfano katika mabadiliko tabianchi.

Jafo anaendelea: "Uwekezaji katika Bwawa la Umeme la Nyerere, ambao zaidi ya shilingi trilioni 6.5 zimewekezwa ili kuja kuzalisha megawati 2,115 na miradi hii yote kimataifa, inaonekana ni miradi ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

Hapo ndipo akirejewa Dk. Samia katika malekezo yake kuhusu mazingira anatamka: "Manufaa ya bwawa hili katika nyanja zote yanawezekana tu kama tutatunza mazingira katika vyanzo vya mabonde ya mito inayoleta maji mabwawani.

"Hapa nataka nisisitize umuhimu wa kutunza mazingira mradi tumeujenga kwa gharama kubwa na kwa kujinyima vitu vingi muhimu itakuwa ni dhambi kubwa kama hautatimiza malengo yake kwa sababu ya uzembe na ubinafsi wetu kwahiyo kulinda mazingira na kulinda mradi huu, sasa ni suala la kufa na kupona,"



Rais Dk.Samia Suluhu Hassan, akiadhimisha siku yake ya kuzaliwa mwaka huu, huko Muwanda Donge, Zanzibar, ambako akashiriki kupanda miti na wananchi wa eneo hilo kutunza mazingira. **PICHA: MTANDAO**

MAZINGIRA

# Tembo 400 wavamia vijiji na kuua wakisimamisha kilimo miaka mitatu

• Askari wanyamapori wapiga kambi vijijini...

**Na Beatrice Philemon**

WAKATI mikoa mingine inafurahia hifadhi misitu na wanyamapori kama kivutio cha utalii katika maeneo yao, wageni wakifika kutoka mataifa mbalimbali na hatimaye kuisaidia Tanzania kupata fedha za kigeni, kijijini Nditi, Kata ya Nditi, wilayani Nachingwea mkoani Lindi, hali iko tofauti.

Malalamiko ya wakazi kijijini ni ushuhuda wa tembo wanavyokuwa kero kwa wananchi, wakivamia makazi ya watu kutafuta chakula na wanapofika wanasukuma baadhi ya nyumba dhaifu, wanaingia ndani wanakula unga.



Sehemu ya tembo waliovamia kijijini Nditi, Nachingwea. **PICHA: MPIGAPICHA**

### ATHARI ZA TEMBO

Mwenyekiti wa Kitongoji cha Njia nne katika kijiji cha Nditi, Rashidi Chilungo, anaisimulia Nipashe namna, wananchi wanavyotaabika sasa, kwamba hali ya chakula ni mbaya, kwani tembo kutoka Pori la Akiba la Selous (Selous Game Reserve) wanavamia makazi na mashamba yao wakila mazao, kitu ambacho hakikuwepo miaka ya nyuma.

Hilo linaendana na hali wanaishi kwenye mazingira magumu, huku kukiwapo jipya la tembo kuingia majumbani mwa watu wakitafuta chakula na maji, baada ya kukosa chakula shambani.

Chilungo anasema kutokana na tatizo hilo, wakazi wa vijiji jirani, sasa wanaiomba serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) iwaongezee angalau askari wa wanyamapori 30 na kuleta helikopta ya kuwafukuza tembo mahali hapo, hata kuwawezesha kurudi mashambani, waendelee na hughuli zao za kilimo na kuishi salama.

"Tunaomba TAWA ituongezee askari wa wanyamapori kwa sababu tembo ni wengi sana, wanazidi kuvamia mashamba yetu na askari waliopo katika kituo ambacho TAWA, imejenga katika kijiji chetu ni wachache sana ukilinganisha na makundi ya tembo ambayo yanavamia kijiji na kuharibu mazao na mashamba ya wananchi," analalamika.

Anasema, kuanzia mwezi Januari hadi Februari mwaka huu, tembo waliongezeka katika kijiji cha Nditi, akitoa hesabu jumla yao 400 kutoka Pori la Akiba la Selous.

Mwenyekiti hiyo anafafanua, athari zinaangukia maeneo kama uharibifu wa mahindi, mihogo, karanga, ufuta, ndizi, korosho, mbaazi ikisababisha janga la njaa, watu kula mizizi ya pori kujihami.

Pia, anafafanua wakulima tajwa wameacha shughuli za kilimo na kuna wengine wanalima mazao kando ya nyumba zao wakihofia kudhuriwa na tembo wavamizi shambani.

> Kuweka askari wa wanyamapori katika kituo hiki kwa ajili ya kufanya doria kijijini, kufukuza tembo kurudi kwenye hifadhi na masuala mengine ya usalama wa wananchi

Chilungo anajitambulisha katika orodha kwamba, yeye ni miongoni mwa wanakijiji katika kata ya Nditi walioathirika na uvamizi wa tembo na kuharibu mazao yao.

Anasema, kabla ya uvamizi wa tembo katika kijiji chao akivuna magunia 25 ya korosho na kupata shilingi milioni tano hadi sita wakati wa msimu wa mavuno, ikimsaidia matumizi ya nyumbani na mengineyo ya kilimo.

"Sasa hivi maisha yangu yamebadilika sana, yamekuwa magumu tofauti na nilivyokuwa natarajia katika mipango yangu. Jumla ya ekari 12 nilizopanda mahindi, ufuta, korosho, mihogo na karanga zote zimeharibiwa na tembo tembo wamekula mazao yote na kung'oa miti yote ya korosho," anasema.

Anatamka, hivi sasa ameamua kuacha kilimo na kuhamia kwenye ufugaji kuku wa kienyeji, zimuwezeshe kupata fedha ya kununua chakula kulisha familia yake. Hadi sasa ana kuku 100 wa biashara.

Mbadala mwingine anautaja ni kufanya kazi ya kibarua kwenye mgodi wa dhahabu uliopo Jirani, ili kujiongezea kipato, baada ya kuona tembo wanazidi kuingia kijijini, wanaharibu mazao na watu hawana chakula, wanaishi kwa mateso ya uhaba wa chakula.

Analalamika sasa njaa imezidi kuongezeka sasa, kwa sababu hivi sasa wanakijiji hawaendi mashambani kulima asubuhi na jioni wanahofia kushambuliwa na tembo wanaoranda kwenye mashamba yao, wakifika hadi majumbani mwao wakitafuta chakula.

Tukio kama hilo lilitokea mwaka 2023 kuanzia mwezi wa Nne na Tano, kundi la tembo kutoka Pori la Akiba la Selous lilivamia vijiji vya Nditi, Namanja, Nambalapala and Nyambi B na kuharibu mazao yote, huku wakiua watu 10.

Inatajwa kati yao, watu nane waliuawa wakiwa nyumbani na wawili mashambani kwao, katika msimu wa kuvuna mahindi.

Pia, inatajwa ilitokea katika vijiji vya Namapwia, Mbute, Kitandi na Nambalapala katika kata ya Luponda mwaka 2023.

### MAFUNZO YA TAWA

Chilungo anaishukuru TAWA kutoa mafunzo kwa wanakijiji na mbinu za kukabiliana na tembo wanaovamia mashamba yao na kuharibu mazao.

"Hadi sasa TAWA imetufundisha jinsi ya kutumia njia za asili kufukuza tembo, kama vile kupiga makopo ili tembo waondoke waende mbali," anatamka Chilungo, akiendeleza mbinu zinazojumuisha:

"Kufuga nyuki kuzunguka shamba, kulima pilipili kichaa, kuzikausha na baadae kuzitwanga ili kupata unga ambao mkulima anatakiwa kumwaga pembeni mwa shamba pande zote,"

Pia, Chilungo anafafanua darasa walilopewa na TAWA, ni mbinu za kumchenga tembo anapowakimbiza kwa chenga za 'zig zaga' na daima wasikimbie kwa kunyooka, wakae mbali na tembo walau wastani mita 100.

"Tunashukuru kupata mafunzo haya kwa sababu baadhi ya wakulima wameanza kulima 'pilipili kichaa' katika maeneo yao na mbegu ya pilipili wanapata kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea, kila mkulima anapata kilo mbili kwa ajili ya kupanda," anasema.

Pia, wananchi wanaiomba serikali iwasaidie kupata eneo lingine kwa ajili ya makazi na kilimo kwa sababu eneo wanaloishi siyo salama tembo wanazidi kuleta hasara.

### MWENYEKITI KIJIJI

Mwenyekiti wa Kijiji cha Nditi, Salumu Husseni anatoa historia, baada ya kuvamiwa na tembo, walipiga simu TAWA kupata msaada.

Anasema, wanakijiji cha Nditi wameathirika sana, kutokana na wanyamapori hao, ikikizingatiwa wananchi wengi wanategemea kilimo cha ufuta, mahindi, mtama, mbaazi, korosho na mazao mengine kama mazao ya chakula na biashara.

Inatajwa mashamba yote yameharibiwa na tembo kuanzia mwezi Januari hadi sasa na kusababisha tatizo la njaa, wananchi wanaishi kwa matumaini hivi sasa.

Anasema takribani miaka mitatu sasa, kijiji cha Nditi wamekuwa wakipitia changamoto hii ya uvamizi wa tembo kuanzia 2022 mpaka sasa.

"Janga hili limekuwa la kitaifa na mimi naamini kuwa mheshimiwa Rais anatambua janga la wanyamapori waharibifu wa mazao na kwenye kijiji hiki nashukuru TAWA imetujengea kituo ambacho kinaitwa 'Problem Animal Control Station'.

"Kuweka askari wa wanyamapori katika kituo hiki kwa ajili ya kufanya doria kijijini, kufukuza tembo kurudi kwenye hifadhi na masuala mengine ya usalama wa wananchi," anasema.

Anasema kupitia askari waliopo kijijini hapo, kumeleta nafu,u kwa sababu wakiona tembo wanakuja kwenye majumba mitaani, serikali ya kijiji inapiga simu askari wanakuja kuwafukuza.

"Tunaomba serikali ituongezee askari wa wanyamapori wengine kama 10 kwa sababu kituo ni kikubwa ili kupambana na tembo hawa ili wananchi waweze kuendelea na shughuli za kilimo na shughuli nyingine za kijamii,' anasema.

### MSEMAJI WA TAWA

Kamishina Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi -Kanda ya Kusini Mashariki-TAWA , Abraham Jullu anasema: "Tuna taarifa kuhusu uvamizi wa tembo katika kijiji cha Nditi na jirani zao baada ya kugundua tatizo hili.

INAENDELEA UK.13

MAZINGIRA

# NEMC yawakusanya wachimba dhahabu wadogo, wawapa darasa la kuacha zebaki

## • Milioni 1.3 waelewa somo, wahamia mbadala

**Na Joseph Mwendapole**

KWA muda mrefu zebaki imekuwa ikitumiwa na wachimbaji wadogo kuchenjua madini ya dhahabu licha ya athari zake mbalimbali za kiafya.

Kwa kuliona hilo, Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), lilikuja na Mradi wa Udhibiti wa Matumizi ya Zebaki kwa wachimbaji hao wadogo na kutafuta teknolojia mbadala wa zebaki.

Kupitia mradi huo, NEMC imefanikiwa kuwafikia wachimbaji milioni 1.3 kwenye mikoa mbalimbali na kuwapa elimu kuhusu teknolojia mbadala ya uchenjuaji wa madini ya dhahabu na matumizi salama ya zebaki.

Mratibu wa Mradi huo, Dk. Betrina Igulu anaiambia Nipashe kuwa, mafanikio yaliyofikiwa mpaka sasa mradi huo ukibakiza mwaka mmoja kukamilika.

Anataja lengo la mradi uliopo ni kuziwezesha nchi wanachama wa Mkataba wa Minamata ambao Tanzania ni mwanachama, ziweze kudhibiti matumizi ya zebaki kwenye uchenjuaji dhahabu.

Dk. Betrina anafafanua kuwa, katika kutekeleza mradi huo, serikali iliandaa mpango mkakati wa kudhibiti matumizi ya zebaki ulioanza kufanyakazi kuanzia mwaka 2020 hadi mwaka 2025.

Anasema, ni mradi wa miaka minne uliopangwa kati ya mwaka 2020 hadi mwaka huu, lakini kutokana na mlipuko wa janga la maradhi Uviko 19, haukuweza kuanza mwaka huo na badala yake ulianza mwaka 2021, kwa matarajio kukamilika mwakani.

Mtaalamu huyo anasema moja ya vipengele muhimu kwenye mradi huo, ni kuwezesha teknolojia mpya mbadala wa zebaki kwa wachimbaji wadogo wa dhahabu hapa nchini.

"Wachimbaji wadogo wengi wanatumia zebaki kama njia rahisi kwao ya uchenjuaji. Sasa sisi wajibu wetu kwenye mradi huu, ni kuwawezesha kujua teknolojia mbalimbali mbadala wanazoweza kutumia, ili waachane na matumizi ya zebaki," anasema



Wachenjuaji madini wakiwa kazini. **PICHA: MTANDAO**

Dk. Betrina anaendelea: "Kwenye maeneo mbalimbali yenye machimbo ya dhahabu tuliyotembelea, wachimbaji walikuwa wakituuliza 'sasa tukiachana na zebaki tutatumia nini?'

### TEKNOLOJIA MPYA

Mtaalamu huyo anasema ndipo walipokuja na majibu ya teknolojia tatu za uchenjuaji dhahabu, bila ya kutumia zebaki.

Hapo anataja jina mojawapo kwa lugha ya kitaalamu 'Concetrration Method' inayohusu uchomaji au kitaalamu inaitwa 'smelting' na matumizi ya kemikali aina ya 'Cyanide' ambayo imeonekana kupendwa na wachimbaji wengi.

Anasema, ili kuhakikisha wanawapatia wachimbaji hao teknolojia mbadala ya zebaki, wamewatambua mafundi mchundo (fabricators) walioko ngazi ya jamii wanaotengeneza teknolojia hizo katika kiwango kidogo kuwawezesha wachimbaji kumudu gharama zote.

Dk. Betrina anataja mafanikio ya mradi huo, ni kuweza kuwaelimisha mamia ya makundi mbalimbali ya wachimbaji wadogo kuhusu teknolojia mbadala katika mikoa ya Mwanza, Geita, Shinyanga, Mara, Singida, Songwe na Mbeya. Ni mahali ambako anataja wamekutana na makundi ya wachimbaji kuelimishana kuhusu matumizi salama ya zebaki na teknojia mbadala wake.

"Miongoni mwa mafanikio makubwa ni pale tulipochukua makundi ya wachimbaji ambao tuliona ni rahisi kwao kuhamia kwenye teknolojia mbadala tukawa tunawatembeza kwenye vituo vyetu vya teknolojia mbadala ili wajifunze na wakafundishe wenzao," anasema

"Tuliwatembeza kwenye vituo vya STAMICO (Shirika la Usimamizi wa Madini) ambavyo tayari vinatumia kemikali ya 'Cyanide' na teknolojia zingine.

"Tulichobaini na hata wenyewe walichotuambia ni kwamba hawakuwa wanajua teknolojia hizi zinapatikana wapi na gharama zake," anafafanua mtaalamu huyo.

Anasema baada ya kuelimishwa, mamia ya wachimbaji wameshaanza kujenga vituo vya kuchenjulia dhahabu kwa kutumia teknolojia mbadala na kwamba matumizi ya zebaki yanaendelea kupungua kila siku.

Anasema serikali haijapita marufuku matumizi ya zebaki, lakini kinachitakiwa ni matumizi salama ili yasisababishe madhara ya afya kwa watumiaji na wananchi wengine.

### SURA MAFANIKIO

Dk. Betrina anataja miongoni mwa mafanikio ya mradi huo, ni kuanzishwa kanuni na mwongozo wa biashara ya zebaki, ambayo awali haikuwepo, hivyo biashara hiyo kuwa inafanywa bila kufuata utaratibu wowote.

Anasema kupitia mwongozi huo, Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, ndiyo inajukumu la kusajili waagizaji wa zebaki na kwamba hilo limefanyika ili kuondoa hali ya olela iliyokuwapo kwenye biashara hiyo.

"Cha msingi sasa, wachimbaji wadogo waache kutumia zebaki zinazopitishwa njia za panya kwa sababu zebaki zinazokuja kwa njia hizo, unakuta nyingi zimeshatumika kwenye nchi zilikotoka kwa hiyo zikiingia hapa zinatumika ndani ya muda mfupi tu na kutupwa tofauti na ambazo hazijatumika ambazo hukaa kwa muda mrefu," anasema

Anasema NEMC imekuwa ikitoa elimu ya madhara ya kuingiza kemikali kinyemela zilizotumika na ambazo hazijatumika kupitia mipaka ya Namanga, Kenya, Tunduma, ,mkoa wa Songwe, pia mkoani Kagera.

Anasema, kupitia Wizara ya Afya wametengeza mkakati wa kulinda afya za watu dhidi ya zabaki uitwao 'Health Prevention Strategy', baada ya kuonekana umuhimu wa kutibu watu ambao wameshapata madhara yatokanayo na matumizi ya zebaki.

"Tulianzisha mkakati huu baada ya kugundua kwamba watu walioathirika na zebaki wakienda kwenye zahanati kupata matibabu wanafanyiwa vipimo kama watu wengine wa kawaida, hali ambayo inawakosesha matibabu sahihi.

Pia, Dk. Betrina anataja mafanikio mengine ya mradi huo kuwa ni kuboreshwa kwa maabara za NEMC na Tume ya Madini kwa kununuliwa kwa vifaa vya kisasa vinavyoweza kupima zebaki ndani ya muda mfupi.

"Kwa mfano kifaa walichokuwa nacho awali ili upate kipimo, ulipaswa kusubiri saa 24, lakini kifaa tulichowanunulia kwa sasa unapata matibu ya kipimo ndani ya saa moja tu kwa hiyo unaweza kuona ni mafanikio makubwa kiasi gani," anasema.

# Tembo 400 wavamia vijiji na kuua wakisimamisha kilimo miaka mitatu

**INATOKA UK.12**

"Tumeamua kusogeza huduma katika kijiji cha Nditi, ili kusaidia wananchi kuishi kwa usalama na wakati huo huo kuwafukuza tembo kutoka kwenye mashamba, mitaani kwenda kwenye Pori la Akiba la Selous."

Kamishna Jullu, anasema hadi sasa TAWA imejenga kituo kwenye kijiji cha Nditi kinachoitwa 'Problem Animal Control Station' na kuweka askari wa wanyamapori wanne, askari wahifadhi wa vijiji wanne waliopata mafunzo kutoka TAWA na kupeleka gari moja la kufanya doria na kufukuza tembo.

Mbali na hilo kila mwezi, TAWA inatoa chakula na posho kwa askari wahifadhi wa vijiji ili waweze kufanya shughuli zao kwa ufanisi.

Pia, jumla ya vijana tisa kutoka kijiji cha Nditi na vijiji Jirani, wapo katika mkoa wa Ruvuma, wakipata mafunzo ya miezi mitatu katika Chuo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii (CBCTC) - Likuyu Sekamaganga kwa ufadhili wa TAWA

Baada ya mafunzo, vijana hao wataungana na wenzao kwenye kituo cha Niti, kata ya Kilamalondo kupambana na tembo wavamizi wa shambani wanaopambana na kuharibu mazao ikiwemo kuua watu .

Pia, inalaezwa TAWA ina mpango wa kujenga kituo kingine katika kata ya Kilimalondo na hadi sasa, kata hiyo imeshatoa jengo na askari wa wanyamapori wanaotumia jengo hilo, kama kituo ili kuwazuia tembo wanaoharibu mazao.

### KAMANDA WA HIFADHI

Kamanda - Hifadhi ya Msanjesi-TAWA, Peter Erro, anazungumzia pilipili kichaa kutumika kwa njia mbili katika kufukuza tembo mashambani:

Hapa anataja njia ya kwanza, ni kutengeneza tofali za pilipili kwa mchanganyiko na kinyesi cha mifugo au tembo. Halafu ikikauka tofali huchomwa shambani au kwenye njia za tembo ambapo ule moshi mkali huzuia tembo.

Pili, anatengeneza uzio ambao pilipili iliyosagwa huchanganywa na 'oili' chafu ikiwekwa vitambaa vidogo, hulowekwa kwa huo mchanganyiko, kisha uzio huwekwa kuzungukia shamba.

AFYA

# Kituo Afya Chanika chamkosha Ummy, mbioni kupandishwa hadhi ya hospitali

## • Akumbusha kliniki presha, kisukari kitaifa

**Na Yasmine Protace**

KUANZISHWA kwa kliniki maalumu za kupima magonjwa yasiyo ya kuambukiza kunatajwa kutazisaidia jamii kuzielewa afya zao.

Ni kauli ya Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu akisema serikali kupitia wizara yake inavitaka vituo vyote vya afya nchini kuanzisha kliniki hizo maalum za kupima magonjwa yasiyoambukiza.

Hapo anataja katika orodha hiyo, ikiwamo kisukari, shinikizo la juu la damu au 'presha', pamoja na kuwapima maradhio ya selimundu (Sikoseli) kwa watoto wanaozaliwa katika vituo hivyo.

Kliniki maalumu za kupima magonjwa yasiyo ya kuambukiza zinapokuwapo katika vituo vyote vya afya nchini, anazitaja kusaidia watu kuzijua afya zao ikiwamo na kuanza kupata matibabu.

Jamii imekuwa ikikumbana na changamoto za kiafya ikiwamo magonjwa yasiyo ya kuambukiza, lakini wengi wao, wamekuwa hawajui kama wana magonjwa hayo.

Anasema, hali ya kuwapo kliniki maalumu ya magonjwa yasiyo ya kuambukiza katika vituo vyote vya afya, kutasaidia hata mwanajamii anapogundulika na magonjwa hayo, atapatiwa elimu juu ya kupambana nayo.

Inatajwa, imekuwa ikichangia kwa kiasi kikubwa baadhi ya watu kupata ulemavu wa kudumu huku wengine kupoteza maisha.



Waziri wa Afya, ummy Mwalimu, alipozuru katika Kituo cha Afya Chanika, nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam, siku chache zilizopita. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

Waziri Ummy anasema, watu hupata ulemavu wa kudumu, pia serikali imekuwa ikiwatibu wagonjwa hao kwa gharama kubwa.

Rai yake ni kwamba jamii ipatiwe elimu juu ya kupambana na magonjwa hayo, ikiwamo stahiki na hata kuchukua taadhari za kujilinda dhidi ya magonjwa na kuyakabili.

Hapo ndipo Waziri Ummy anasisitiza kwamba, kunapokuwapo kliniki maalumu na jamii husika ikaelewa umuhimu wake, ni jambo analolitaja litasaidia jamii kujitambua, kwa kupatiwa matibabu yatakayomsaidia mgonjwa asitesake.

### ALIPOTIA MGUU CHANIKA

Katika ziara yake katika Kituo cha Afya Chanika, nje kidogo ya jiji la Dar es Salaam, Waziri Ummy akilenga hali ya utoaji huduma, hata akatoka akikiri karidhishwa na huduma za afya zinazotolewa mahali hapo.

"Nawapongeza sana wataalamu wa kituo hiki cha Afya cha Chanika kwa huduma nzuri mnazozitoa, pia kuwa na kliniki za magonjwa yasiyoambukiza.

"Sasa hivi tunataka kuona kila kituo cha afya nchini kuwa na kliniki za magonjwa hayo, husan upimaji wa ugonjwa wa kisukari, shinikizo la juu la damu pamoja na sikoseli," anasema.

Anaongeza kuwa watoto wanaozaliwa na ugonjwa wa sikoseli, wanapoanza kupata matibabu mapema, inawasaidaa kuondoa fikra potofu kwa baadhi ya wazazi, kwamba zinaaamabata na imani za kishirikina.

Waziri anaeleza kuwa, wapio wazazi wanaodhani kwamba watoto wao wamerogwa kwa kuwa mtoto asipogundulika mapema, huwa anaumwa kila mara.

Ummy anaeleza, pia miondombinu ya majengo itaongezwa katika Kituo cha Afya Chanika, ili kupadishwa hadhi na kuwa hospitali ya ngazi ya kwanza, kwa kuwa kituo hicho kinafanya kazi kubwa ya kuwahudumia wananchi wengi zaidi.

"Katika kituo hiki kwa siku wanatoa huduma za kuzalisha wanawake 30 hadi 50 kwa siku, hali ambayo ukifananisha na baadhi ya hospitali za wilaya, idadi hiyo ndio wanaozalishwa kwa mwezi," anasema.

Anasema kituo hicho kwa mwezi kinahudumia wagonjwa kati ya 700 hadi 800, ambayo ni kazi kubwa na nzuri inayofanyika mahali hapo.

Mganga Mkuu wa Jiji la Dar es Salaam, Dk. Zaituni Hamza, anaishukuru serikali akaipongeza Wizara ya Afya kwa kuendelea kuwatia moyo watumishi wa afya na kuthamini wanachokifanya hasa kutoa huduma bora kwa wateja.

"Tunamshukuru Mheshimiwa Waziri kuelekeza kituo hiki kuwa na hadhi ya hospitali, baada ya kukamilisha vigezo vilivyobakia ikiwamo kuongeza baadhi ya majengo.

"Kituo hiki kikiwa hospitali, kitasaidia kupunguza msongamano wa wateja kwenda katika hospitali nyingine kama Muhimbili na Amana," anasema Dk. Zaituni.

## SIKU YA WANAWAKE DUNIANI...

# Mkuu UWT awasha moto Songwe kisa ulawiti, ubakaji kunavyokithiri

**Na Ibrahim Yassin,** Songwe

KUNAELEZWA kuwapo tabia ya kinamama kuwaficha watoto wao waliokumbwa na tatizo la unyama wa ama kubakwa au kulawitiwa na watu wazima, wakiwamo ndugu kuepuka aibu.

Hata hivyo, inatajwa wanaangukia kukosa misaada mbalimbali, ikiwamo kisheria, huku kasi ya ubakaji, ulawiti na unyanyasaji kijinsia unazidi kushika kasi katika jamii nchini na wanaoendesha vitendo hivyo ni ndugu watu wa karibu.

Mgeni rasmi kwenye maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani mkoani Songwe, Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Taifa (UWT) Mary Chatanda, anaeleza kusikitishwa na wanaume watu wazima kuwabaka na kuwalawiti watoto.

Inatajwa wengi hufanya hivyo, katika imani ya kishirikina kupata tenda na utajiri mwingineo na fedha nyingi ziwafikie kibiashara, kilimo, uchimbaji madini na ufugaji, unaoenda kwa waganga wa kienyeji na kuambiwa wakabake mtoto wadogo.

Chatanda analalamika kukithiri ubakaji na ulawiti kumetokana na wazazi au malezi kutokuwa karibu na watoto wao, wengi waangalia kazi zao ama biashara bila kujua mienendo ya watoto,na pia masuala ya utandawazi ndiyo yanaharibu zaidi watoto.

Pia, anatoa rai kwa wazazi na walezi kuacha kuwalaza chumba kimoja watoto wa kiume na kike na hata ndugu wa jinsia furani wanapokuja kusalimia nyumbani wasiwalaze pamoja na watoto wa jinsia tofauti ili kukwepa ubakaji.



Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), alipokuwa katika Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Tanzania, mkoani Songwe. **PICHA: IBRAHIM YASSIN**

Anasema, watu hao wanafanya hivyo kwa ajili ya ushirikina wa kupata mali kwani mitaani waku bwa wenzao wapo, lakini wanaendekeza kuwaharibu watoto,hivyo amewatangazia kiama na kulitaka jeshi la polisi kuliangalia hilo kwa jicho la tatu.

"Nchi nzima imekumbwa na malezi mabaya kwa Watoto. Kumekuwa na vitendo vya kikatili vya ubakaji na ulawiti vinavyosaba bishwa na ndugu wa karibu.

"Utandawazi ni moja ya viashiria vya mmomonyoko wa maadili jamii inatakiwa kuwalea watoto kwa misingi ya utamaduni za Kitanzania," anasema.

Mkuu huyo wa UWT, anasema ni kwamba mbali na kukemea vitendo vya unyanyasaji kijinsia, akiwasisitiza wanaume kuacha kuharibu watoto wadogo.

Anaendelea kwa tahadhari: "Wazazi tumejisahau, acheni kuwapa simu watoto, wakiwarubuni kuwa wanacheza gemu kumbe wanaangalia mambo ya kikubwa (ngono) na baadae wanawatafuta vijana kujaribu tendo hilo na kujikuta wakiharibikiwa."

Chatanda anamsifu Rais Dk. Samia Suluhu Hassam, kwamba amejitahidi kujenga shule nyingi, lakini bado maadili ya watoto wanaharibikiwa kimaadili shule hizo anahiji 'atasoma nani?'





# Waziri ahimiza usimamizi fedha miradi

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

WAZIRI wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, amewasisitiza wasimamizi wa miradi yote ya ujenzi ya serikali inayotumia utaratibu wa 'force account' kuimarisha usimamizi ili wazawa wapate nafasi ya kumiliki uchumi.

Dk. Nchemba alitoa agizo hilo jana kwenye hafla ya kuweka jiwe la msingi la Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) Tawi la Dodoma, jijini hapa.

Aliwataka wasimamizi hao wa miradi kuimarisha usimamizi wa fedha zote za miradi hiyo zinazotolewa na serikali ili kuwanufaisha wazawa na kukuza uchumi wa nchi.

"Nimepewa taarifa hapa kuwa mnatekeleza ujenzi wa miradi yenu yote kwa kutumia 'force account' na imeonyesha mafanikio. Nawataka wasimamizi wote wa miradi yote nchini kusimamia fedha hizo vizuri ili kuwawezesha wazawa kiuchumi," alisema.

Pia alisema miradi hiyo inayotekelezwa na chuo hicho kama wangetumia makandarasi, fedha zingetumika nyingi tofauti na zile zilizotumika kujenga majengo hayo.

Chuo hicho, alisema kimeonyesha utaratibu huo unavyoweza kutekelezwa na kuipunguzia serikali gharama za ujenzi. Pia aliwataka wasimamizi hao kuhakikisha majengo yanakuwa na thamani halisi ya fedha za walipakodi zilizotumika.

Awali, Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Eliaman Sedoyeka, alisema chuo hicho ambacho makao makuu yake yako Arusha, kina matawi matatu ambayo ni Dodoma, Babati na Dar es Salaam na wanatarajia kufungua tawi lingine mkoani Ruvuma.

Prof. Sedoyeka alisema chuo hicho kilifungua tawi Dodoma mwaka 2021 na wamekuwa wakitumia majengo ya kukodi lakini wameona umefika muda wa kujenga jengo lao ili kupunguza gharama za uendeshaji.

Kwa mujibu wa Prof. Sedoyekam jengo hilo litatumia Sh. bilioni 5.08 na litakuwa na ghorofa sita. Hadi sasa, alisema Sh. bilioni 1.7 zimetumika kugharamia ujenzi huo.

Aliongeza kuwa chuo kimejenga na kinaendelea na ujenzi wa majengo mengine katika kampasi kuu Arusha na tawi la Babati na Sh. bilioni 48 zimetengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Prof. Seoyeka alisema hivi sasa wanakabiliwa na tatizo la kupata eneo la chuo kwa Dar es Salaam ili kujenga majengo ya kudumu na kumwomba waziri kuwasaidia kupata eneo kwa sababu fedha za kujenga zipo.



Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba (kushoto), akikagua ujenzi wa jengo la Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA), tawi la Dodoma, katika eneo la Njedegwa juzi, baada ya kuweka jiwe la msingi. Wengine ni Mkuu wa chuo hicho, Eliaman Sedoyeka (kulia) na (wapili kulia) ni Mbunge wa Arusha, Mrisho Gambo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## Wapongeza kufufuliwa chuo baada ya miaka 20

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii imeishukuru serikali kwa kufufua chuo cha ufundi stadi na marekebisho kwa watu wenye ulemavu Rwenzari mkoani Tabora ambacho kilikuwa hakifanyi kazi takriban miaka 20.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Fatuma Toufiq, alisema hayo jana mkoani Tabora katika ziara ya kamati kukagua maendeleo ya chuo hicho.

Alisema serikali imedhihirisha dhamira yake ya kuhakikisha makundi ya watu wenye ulemavu wanapata fursa sawa za kushiriki katika kujenga taifa lao na kuishi katika mazingira salama.

Pia alisema mafunzo wanayopata wanafunzi chuoni hapo yatawasaidia kujiajiri na kuanzisha mafunzo kwa watu wengine ili kuinua uchumi wao na Taifa kwa ujumla.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, alisema miongono mwa maboresho yaliyofanyika ni pamoja na ununuzi wa samani, upanuzi wa kuta na vifaa kwa ajili ya wanafunzi kujifunzia.

Awali, Kaimu Katibu Mkuu Ofisi hiyo ambaye ni Mkurugenzi wa Sera na Mipango, Saidi Mabie, alisema serikali ilitoa Sh. milioni 689 kwa ajili ya kukarabati chuo hicho ambacho kina uwezo wa kuchukua wanafunzi 129 katika kozi za uselemala, ubunifu ushonaji, kilimo bustani, uchomeleaji na umeme wa majumbani.

Mwanafunzi wa chuo hicho, Amos Yokram, aliishukuru serikali kwa kuendelea kuwajali watu wenye ulemavu na kuboresha miundombinu kwa ajili ya kupata elimu.

## Dendego apiga marufuku kusikia 'changamoto'

**Na Elisante John,**
SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, amesema katika uongozi wake hataki kusikia neno 'changamoto' kwa watumishi kwenye utekelezaji wa miradi ya maendeleo mkoani humo kwa kuwa ni moja ya sababu zinazokwamisha shughuli za maendeleo.

Dendego ambaye amehamishiwa mkoani hapa kutoka Iringa, alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na watumishi baada ya kukabidhiwa ofisi na mtangulizi wake, Peter Serukamba, ambaye amehamishiwa Iringa.

Alisema ni lazima kazi zifanyike na majibu yapatikane kupitia utumishi huku akisisitiza atakuwa msikivu, mnyenyekevu na mtulivu katika kuongoza na kusimamia shughuli za maendeleo ya mkoa.

Awali, Serukamba alizishukuru kada mbalimbali za uongozi tangu alipowasili mkoani Singida mwaka mmoja na miezi saba iliyopita na kusema amejifunza mengi ya maendeleo atakayoyaendeleza alikohamishiwa.

Alisema akiwa Singida anajivunia kupandisha matumizi ya mbolea ikilinganishwa na hali aliyoikuta, huku pia akifanikisha upatikanaji wa mbegu ya ruzuku ya alizeti.

Serukamba alisema anajivunia kumaliza tatizo la mauaji lililoikabili wilaya ya Manyoni ambalo lilikithiri nyakati za usiku kwa ufukuaji wa makaburi kutokana na imani za kishirikina.

Akizungumza kwa niaba ya Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Singida, Katibu Mwenezi wa CCM Mkoa, Eliphas Lwanji, aliahidi kuwa chama CCM na serikali ya mkoa kumpa ushirikiano wa kutosha mkuu huyo mpya wa mkoa ili atekeleze majukumu yake kwa ufanisi.

## Aonya ongezeko maradhi ya figo

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

MKURUGENZI Mtendaji wa Hospitali ya Benjamin Mkapa (BMH), Dk. Alphonce Chandika, amesisitiza mtindo bora wa kula kutokana na tatizo la figo kwa kuwa sasa ni tishio.

Katika hospitali hiyo, kila siku wagonjwa 50 wenye tatizo la figo husafisha damu katika kitengo cha kusafisha damu katika Idara ya Magonjwa ya Figo.

Akizungumza jana ikiwa ni Siku ya Figo Duniani, Dk. Chandika alisema wananchi wanapaswa wafanye mazoezi kuzingatia mlo usioathiri moyo ili kuzilinda figo.

"Wananchi tuwe na mtindo bora wa maisha unaozingatia milo isiyoathiri moyo utaisaidia kuzilinda figo kauli mbiu ya mwaka huu ya siku ya figo ni afya ya figo kwa wote pamoja na upatikanajibora wa matibabu," alisema.

Alibainisha kuwa hadi sasa hospitali hiyo imeishafanya oparesheni za upandikizaji figo kwa watu 36 tangu huduma hiyo ianze miaka sita iliyopita.

Alisema jamii inapaswa kuzingatia ushauri wa wataalam unatolewa kwa wananchi ili kulinda afya zao.

Hata hivyo, Dk. Chandika aliwataka wananchi kujitokeza hospitalini pale wanapoona wana dalili zote za magonjwa ya figo ili wapatiwe matibabu kabla ugonjwa haujawa sugu.

Alisema wengi wao wamekuwa wakikaa nyumbani na matokeo yake wanafika hospitali tatizo likiwa kubwa ndipo wanaanza matibabu kutoka kwa wataalamu.

"Jamii iweke utaratibu wa kuhudhuria hospitali kila mara kujua nini kinawasumbua katika miili yao, wasikae nyumbani kujiuguza na miti shamba, tatizo la figo linatibika,"alisema.





# Kamati: Rais Samia amesogeza nyenzo, utendaji haki kwa jamii

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, imesema Rais Samia Suluhu Hassan amesogeza nyenzo na miundombinu ya utendaji haki kwa Watanzania, ikiwamo Mahakama na vifaa vya Tehama ili kurahisisha huduma kwa wananchi.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Joseph Mhagama aliyasema hayo wakati wa ziara ya kukagua ujenzi wa vituo vya haki jinai pamoja na ugawaji vifaa vya Tehama katika magereza ya wilaya za Njombe na Ludewa mkoani Njombe.

Mhagama alisema kusogezwa kwa nyenzo hizo kutakwenda kuboresha maisha ya Watanzania.

Alisema kuwa kamati hiyo inampongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa uwekezaji mkubwa ambao ameufanya ambao unakwenda kuboresha maisha ya Watanzania.

Alisema: "Iliratibiwa wakati fulani na Ofisi ya Mkurugeni wa Mashtaka kutoka na kukosekana kwa muda lakini sasa mmekwenda kuwekeza huko na kuna changamoto mbalimbali ambazo tulitamani tuzijue ili tuweze kuishauri serikali".

Alisema awali waliangaika kutafuta bajeti ya DPP ili kuharakisha mashauri kwa sababu ya mrundikano wa mahabusu lakini ilibainika kuna changamoto za miundombinu ambazo hazikidhi mahitaji ya baadhi ya mahabusu aidha kwa kuzingatia jinsia zao au kwa kuzingatia jinsi.

Waziri wa Katiba na Sheria, Balozi Dk.Pindi Chana alisema Gereza la Wilaya ya Njombe limepatiwa seti ya televisheni ya kuendesha mikutano ya mahakama ikiwemo kamera moja kompyuta mpakato moja na kompyuta ya mezani moja.

Hivyo aliishukuru kamati hiyo kwa mfumo wa uendeshaji kesi kwa njia ya televisheni, akisema kwa sasa hivi wanakwenda kwenye Tehama.

Dk. Chana alisema thamani ya bajeti ya ununuzi wa vifaa hivyo imegharimu kiasi cha Sh. milioni 600.



Waziri wa Mambo ya Ndani, Mhandisi Hamad Yusuf Masauni (wa pili kushoto), akiwa na Mkurugenzi wa Oryx Gas Tanzania, Benoit Araman (kushoto), wakimkabidhi mtungi wa kupikia wa gesi wa Orxy, Adhuruu Makame Kombo, katika hafla ya ugawaji wa mitungi 700 ya kupikia kwa babalishe na mamalishe katika viwanja vya Mnazi Mmoja, Zanzibar jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Baba, mama lishe wapewa msaada mitungi ya gesi

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI serikali ikiendelea kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia, Waziri wa Mambo ya Ndani, Mhandisi Hamad Yusuf Masauni, kwa kushirikiana na kampuni ya gesi ya Oryx wametoa msaada wa mitungi 700 ya gesi kwa wajasiriamali.

Akizungumza wakati wa ugawaji wa mitungi hiyo, Waziri Masauni alisema Rais Samia Suluhu Hassan pamoja na Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi wamekuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Alisema kitendo cha Oryx kushirikiana naye kugawa mitungi hiyo bure kwa wananchi wa Kikwajuni kunakwenda kusaidia kuifanya jamii hiyo kuachana matumizi ya kuni na mkaa.

"Tunaamini waliopata majiko haya ya gesi pamoja na kupatiwa mafunzo ya namna ya kuyatumia watakuwa mabalozi wazuri kwa kuwahamasisha wananchi wengi zaidi wa Zanzibar na Tanzania wahame kutoka katika matumizi ya kuni na mkaa na waje katika kutumia gesi," alisema Masauni.

Alisema wajasiriamali waliopata mitungi hiyo kwa awamu ya kwanza ni 700 na malengo ni kuwafikia wajasiriamali 24,000 wa Kikwajuni.

Mkurugenzi wa Oryx Gas Tanzania, Benoit Araman alisema wanaamini mwananchi akipika kwa kutumia gesi, inaleta maendeleo kwa jamii sambamba na kulinda mazingira kwa kuacha kukata miti.

Alisema: "Zaidi ya yote ni kulinda afya ya wanawake kwa kuwaepusha kuvuta moshi na mvuke unaoathiri mapafu na afya yao unaotokana na kuni na mkaa. Hivyo tunakushuru Waziri Masauni kwa kushirikiana nasi katika kuhakikisha wananchi wa Kikwajuni wanapata niashati safi ya kupikia."

Alisema kwa miaka mingi Oryx Gas imekuwa kampuni kiongozi katika kukuza matumizi ya gesi nchini Tanzania na kuanzia Julai, 2021 wamekuwa mstari wa mbele kutekeleza maelekezo ya serikali.

Alisema wanajipongeza kwa kujulikana kuwa kampuni kinara katika usambazaji wa gesi ya kupikia kwa Watanzania kwa sasa na kwamba wataendelea kuwekeza zaidi katika kueneza nishati safi kutumika kwa wananchi wengi.

Aidha alimshukuru Waziri Masauni kwa kuwa balozi mzuri wa kuleta maendeleo kwa jamii kwa kuwaunga mkono katika mpango wa matumizi ya nishati safi.

Wakati huo huo, Meneja Masoko wa Kampuni ya Oryx Gas, Peter Ndomba pamoja timu nzima ya kampuni hiyo wametoa mafunzo ya matumizi ya nishati safi ya kupikia, lengo likiwa kuiwezesha jamii kuwa salama na kuepuka madhara yanayoweza kutokea wakati wa kutumia majiko ya gesi.

## Watu 178 mbaroni tuhuma za wizi, mauaji

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

JESHI la Polisi mkoani Njombe limewakamata watu 178 ambao wanatuhumiwa kujihusisha na matukio ya wizi pamoja na mauaji.

Akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi Mahamoud Banga alisema msako huo ulifanyika Februari mwaka huu.

"Tumefanikiwa kukamata runinga nne, pikipiki moja, betri moja ambayo inatumia sola, tairi moja kubwa, king'amuzi, spika za redio vilevile tumefanikiwa kukamata powermixer moja," alisema Kamanda Banga.

Alisema Jeshi la Polisi katika operesheni hiyo imefanikiwa pia kuwakamata watu wawili John Kato (50) pamoja na Shabani Karoli ambao wanatuhumiwa kujihusisha na tukio la kuvunja ghala la kuhifadhia vifaa vya ujenzi.

Kamanda Banga alisema Jeshi la Polisi limejikita katika kutoa elimu kwa madereva wa magari ili kuhakikisha kwamba wanatumia vizuri barabara.

Aidha alitoa wito kwa wananchi mkoani Njombe kufuata sheria, kwamba Jeshi la Polisi haitawafumbia macho watu wote wanaojichukulia sheria mkononi.

## Wapewa kongole utunzaji vyanzo vya maji, kupanda miti

**Na Elizabeth John,** MAKETE

WANANCHI wa Kata ya Lupalilo wilayani Makete mkoani Njombe, wamepongezwa kwa kutunza vyanzo vya maji pamoja na kupanda miti kwenye vyanzo vya maji.

Ofisa Mazingira wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete, Upendo Mgaya, alitoa pongezi hizo wakati wa upandaji miti katika chanzo cha maji Ng'usi.

Alisema vyanzo vya maji vinafaida kubwa kwa nchi kwa kuwa vinatiririsha maji katika Bonde la Rufiji na Bonde la Ziwa Nyasa ambalo kuna miradi mikubwa ya serikali.

Ofisa Misitu wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete, Naferi Sanga, aliwataka wananchi kuendelea kutunza vyanzo vya maji kwa kutofanya shughuli zinazoharibu mazingira.

Mtendaji wa Kata ya Lipalilo, Sabas Kereth, alisema suala la kupanda miti ni agenda katika kata hiyo ili kutunza mazingira.

"Suala la kupanda miti ni agenda yetu kwa hiyo wito wangu kwa wananchi ni kuitunza miti hii ili iweze kuleta tija kwa vizazi vya sasa na baadaye," alisema Kereth.

Baadhi ya wananchi waliojitokeza katika shughuli hiyo, akiwamo Janeth Mhagama, alisema wapo tayari kulinda miti na kwamba wataelimishana kuhusu kutopeleka mifugo katika eneo hilo.

Zaidi ya miti 9,000 imepandwa katika chanzo hicho cha maji ikiwa ni mpango mkakati wa kutunza mazingira.



## Mfumuko wa bei waleta ahueni mwezi Februari

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KASI ya kiwango cha mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia Februari 2024, imeshuka hadi asilimia 5.10 kutoka asilimia 5.26 iliyorekodiwa Januari 2024.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Kitengo cha Takwimu za Bei Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Salma Saleh Ali, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari, Mazizini jana.

Alisema, kushuka kwa kiwango cha mfumko kulichangiwa zaidi na kushuka kwa bei za bidhaa za vyakula na vinywaji visivyo na vileo kwa asilimia 8.66 Februari 2024 ikilinganishwa na asilimia 8.98 mwezi Januari.

Alisema, faharisi za bei zimeongezeka kufikia 109.53 mwezi Februari 2024 ikilinganishwa 104.22 Februari, 2023.

Aidha, mfumko wa bei wa bidhaa za chakula wa mwaka ulioshia Februari 2024 umepungua na kufikia asilimia 8.88 ikilinganishwa na asilimia 9.21 iliyorikodiwa mwezi Januari 2024.

Alisema, faharisi za bei za chakula kwa mwezi Februari 2024 ziliongezeka na kufikia 116.83 kutoka 107.30 katika mwezi Januari 2023.

Mfumuko wa bei wa bidhaa zisizo za chakula kwa mwaka umepungua na kufikia asilimia 2.40 kwa mwezi Februari 2024 ikilinganishwa na asilimia 2.46 katika mwezi wa Januari 2024.

"Faharisi za bei za bidhaa zisizo za chakula zimeongezeka na kufikia 104.56 kwa mwezi Februari 2024 ikilinganishwa na asilimia 102.11 katika mwezi Februari 2023.

Alizitaja bidhaa zilizosababisha kupungua kwa mfumuko wa bei ni pamoja na mchele wa Mbeya (11.0%), unga wa ngano (4.2%), unga wa sembe (5.5%), ndizi za mtwike (25.5%), na mafuta ya kula (6.7%).

Meneja Msaidizi, Uchumi Benki Kuu, tawi la Zanzibar, Shami Chamicha, alisema kupungua kwa kasi ya mfumuko wa bei ni hatua nzuri ya kiuchumi na malengo yaliyopo ni kubakia kwenye tarakimu moja.

"Ni ahueni kwa wananchi na hii inatokana na kuwapo kwa bidhaa za kutosha kwenye masoko. Lakini kwa ujumla hali ya uchumi imeendelea kubakia vizuri na hata upatikanaji wa dola hivi sasa upo vizuri," alisema.

Mchumi Mkufunzi Mwandamizi Skuli ya Biashara, Dk. Estella Ngoma Hassan, alisema kushuka huko kwa kiwango cha mfumuko ni hali ya kawaida kulingana na mwenendo wa kibiashara.

Aidha, alisema kuwapo kwenye tarakimu moja ni njia bora ya kuwavutia wawekezaji kwa ajili ya kuwekeza nchini kwa maendeleo ya taifa.

# Waliofariki dunia kwa kula kasa wafikia tisa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

IDADI ya waliofariki kwa kula nyama ya kasa kisiwani Pemba imeongezeka na kufikia watu tisa.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari jana visiwani Zanzibar, Naibu waziri wa Afya, Hassan Khamis Hafidh, alisema kuwa idadi ya walioripotiwa kupata madhara kwa kula kiumbe hicho imeongezeka na kufikia watu 160.

Alisema waliofariki ni watoto chini ya umri wa miaka 10 na bado watu 18 kati ya 160 waliopata madhara wanaendelea kupatiwa matibabu katika hospitali ya Abdallah Mzee, kisiwani Pemba.

Alisema tukuo hilo limetokea Machi 6, mwaka huu katika Kijiji cha Kisiwa Panza, Kusini Pemba.

Hafidh alisema Wizara ya Afya imepiga marufuku ulaji wa nyama wa kiumbe huyo wa baharini ambaye huwa na sumu kali kutokana na vyakula wanavyokula wakiwa baharini.

"Wizara ya afya inawapa pole wale wote waliokula nyama hiyo na wale waliofariki. Niwaombe wananchi kuachana kabisa na ulaji wa kasa," alisema.

Alisema kuna aina saba ya kasa na kati ya hizo aina nne huwa ni hatari na wana madhara, hafai kuliwa lakini ni vigumu kumgundua kasa mwenye sumu kati ya aina hizo saba.

Mkemia Mkuu wa Serikali, Dk. Faridi Mzee Mpatani, alisema kasa ana sumu inayotokana na aina ya majani na matumbawe yaliyopo baharini.

Alisema katika uchunguzi wamegundua kuwa sumu hiyo husababisha madhara katika mfumo wa ufahamu wa binadamu na husababishwa na mimea na vimelea vya baharini ambavyo hutumiwa na kasa kama chakula chao.

Alisema madhara ya sumu hiyo humsababishia binadamu kukosa nguvu, kupata ganzi, kutapika na kuharisha na kufariki dunia na kwamba watoto chini ya miaka 15 huwaathiri zaidi.

Alisema kuna baadhi ya viumbe baharini wanaweza kula mimea yenye sumu hiyo na wasilete madhara kwa binadamu.

Naibu Mkurugenzi kinga na elimu ya afya wa Wizara ya Afya, Fatma Mohamed Kabole, alisema wagonjwa hao pamoja na waliofariki ni kutoka katika familia tofauti.

Alisema baada ya kupata taarifa hiyo walifuatilia na kufika katika familia hizo na kugundua baadhi ya wagonjwa wamefichwa majumbani.

"Yawezekana idadi ya walioathirika wakaongezeka kwa sababu wananchi wanaficha taarifa ya waliokula nyama hiyo," alisema.

Hata hivyo, alisema Wizara ya Afya inaendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu kuacha kula viumbe vya baharini vyenye madhara ikiwamo kasa na bunju kwa sababu hakuna tiba ya kudhibiti sumu ya viumbe hao.

Imedaiwa kuwa baadhi ya watu wanaokula nyama hiyo wanaamini inaongeza nguvu za kiume.



Mkemia Mkuu wa Serikali Zanzibar, Dk. Farid Mzee Mpatani akitoa taarifa ya kitaalamu, jijini Zanzibar juzi, kufuatia vifo vya watu 9 vinavyosadikiwa kusababishwa na kula nyama ya kasa Machi 6 mwaka huu huko Kisiwa cha Panza, Pemba. **PICHA: MAELEZO ZNZ**

# Othman afurahishwa fursa kupambana na Ukimwi

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema ni fursa muhimu kwa nchi kuwapo na mpango endelevu wa kitaifa katika kuendeleza juhudi za pamoja na washirika wa maendeleo kupambana na maambukizo na maradhi ya Ukimwi.

Othman aliyasema hayo juzi ofisini kwake Migombani mjini Zanzibar alipozungunza na ujumbe wa washirika wa wa maendeleo uliongozwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kupambana na Ukimwi Duniani (UNAIDS), Mfumo wa Rais wa Marekani pamoja na Taasisi ya Marekani ya kudhibiti maradhi mbali mbali.

Ujumbe huo ulikuwa na dhamira ya kumweleza Makamu azma ya mashirika hayo na umuhimu wa nchi kushirikiana nayo kuisaidia Zanzibar kuwa na mpango endelevu wa kupambana na maambukizi ya virusi vya Ukimwi na Ukimwi.

Alisema, kuwapo kwa mpango huo kutaisadia Zanzibar kupiga hatua na kuwapo mafanikio mazuri ya vita dhidi ya janga la maradhi ya Ukimwi na kusaidia kufikia lengo la kimataifa la kumaliza matatizo ya Ukimwi ifikapo mwaka 2030.

Alisema jitihada zanazofanywa na serikali katika vita dhidi ya janga hilo zimesaidia kuwapo mafanikio makubwa na mpango huo utaongeza nguvu ya Zanzibar kuelekea mafanikio makubwa zaidi ya mapambano ya maradhi hayo.

Aidha, alisema nchi haiwezi kupambana na janga la Ukimwi kwa kubakia na kuendeleza mpambano hayo kwa kutumia mtindo na mbinu za mazoea na kwamba kuwapo kwa mpango huo ni jia bora ya kufikiri katika kumaliza tatizo la Ukimwi Zanzibar. Hata hivyo, alisema licha ya kuwapo mafanikio ni muhimu njia na mbinu mbadala za kuwezesha mafanikio zaidi ya mapambana na hali ya mambukizi ya maradhi ya Ukwimi na kuyadhibiti.

Alisema Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imevutiwa na washirika hao wa maendeleo katika kufikiria mpango huo hasa kwa vile utasaidia kuutumia uzoefu uliotumiwa na mataifa tofauti na kuelewa changamoto mbali mbali zilizowakumba.

Mshauri wa Shirika la Umoja wa Matifa la kupambana na Ugonjwa wa Ukimwi Duniani (UNAIDS) Dk. Gorge Loy, alisema washirika wa maendeleo wa kupambana na maradhi hayo wataendelea kushirikiana na Serikali ya Zanzibar kuandaa na kuwapo na mpango endelevu utakaotumika kumaliza tatizo la Ukimwi Zanzibar.

Alisema katika kuandaa mpango huo serikali chini ya usimamizi wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inatakiwa kuunda kamati ya kitaifa ya kitaalam watakaokuwa na jukumu la kuandaa mpango huo endelevu ili kumaliza matizo ya Ukimwi nchini.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Fedha na Mipango Zanzibar, Dk. Saada Mkuya, alisema kamati hiyo itasaidia kuyakabili mazingira tofauti ya kupambana na tatizo la Ukimwi nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa Tume ya Ukimwi Zanzibar, Dk. Ahmed Khatib, alisema mpango endelevu wa kupambana na Ukimwi Zanzibar ni shirikishi kwa jitihada za wadau tofauti wa maendeleo kama ni jitihada ya pamoja ya kupamba ikiwamo Shirika.

# **MATANGAZO** MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**NANCY DANIEL KAMALA** anatangaza kupotelewa na hati ya kusafiria yenye namba **TAE181700** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Makao Makuu. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Control number: **9910840455266.**

## KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI

**BETSON ALAM MAHENGE** anatangaza kupotelewa na kadi ya Bajaji yenye namba za usajili **MC 754 AEE.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **MKO/RB/480/2024.**

## TANGAZO LA KADI YA GARI KUPOTEA

**Ndugu HASSANI HAMISI HERY** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **Toyota Corona** yenye namba za usajili **T212 ASR,** Yenye Chassis namba 190410914 ilisajiliwa kwa jina la **Mohamed Ahmed Habib.** Kwa yeyote atakayeiona anaombwa atoe taarifa kituo chochote Cha polisi kilichopo karibu nae. Taarifa ya polisi **PHQ/TAN/TAN/3774/2023.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**GOODLUCK WILLIAM MSANGI** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 290 AER** **Toyota Hiace.** Chasses Namba **YH7106001071,** Engine Namba **3Y0229923** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi Taarifa: **PHQ/KIL/ MWA4339/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PETER AMOS MALEKELA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **Suzuki ESCUDO,** yenye namba za usajili **T 762 CNK,** Chassis No.***TD01W131580,*** Engine No. G16A531105. Yeyote atakaeiona atoe taarifaN kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/6946/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NATALIA WATSON MWAIGAGA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 682 DHJ – TOYOTA COASTER.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya **Polisi: MKO/RB/36/2024.**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(DAR ES SALAAM DISTRICT REGISTRY)**
**AT DAR ES SALAAM**
**TAXATION NO. 198 OF 2023**
**(Arising from Civil Land Case no. 2023)**
**INTERNATIONAL COMMERCIAL............DECREE HOLDER**
**VERSUS**
**URAFIKI TRADING AGENCIES......1ST JUDGMENT DEBTOR**
**AUNALI KASSAM......................... 2ND JUDGMENT DEBTOR**
**ABASALI AUNALI KASSAM.........3RD JUDGMENT DEBTOR**
**SAKKIR ALI KASSAM...................4TH JUDGMENT DEBTOR**
**KASSAM ALI AKBERALI KASSAM......5TH JUDGMENT DEBTOR**

**KUITWA SHAURINI**

**KWA: URAFIKI TRADING AGENCIES, AUNALI KASSAM, ABASALI AUNALI KASSAM, SAKKIR ALI KASSAM, KASSAM ALI AKBERALI KASSAM – DAR ES SALAAM.**

Kwa kuwa mdai aliyetajwa hapo juu amefungua maombi ya gharama za shauri la madai Na. 198/2023 dhidi yenu, shauri ambalo maelezo yake yameelezwa katika nakala za hati za madai zinazopatikana katika Mahakamani hii, kwa hiyo mnatakiwa kuhudhuria katika Mahakama hii nyie wenyewe au Wakili au mwakilishi wenu anayeruhusiwa kisheria, siku ya tarehe **18/3/2024** saa nne (4:00) kamili asubuhi mbele ya **S.B. FIMBO NAIBU MSAJILI** kujibu madai dhidi yenu. Mnaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo mnatarajia kuvitumia katika utetezi wenu siku hiyo.

**ANGALIA:** Kama msipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kuwa mmepokea taarifa hii ya kuitwa shaurini, basi shauri linaweza kusikilizwa na kuamuliwa bila uwepo wenu.

**HATI** hii imetolewa kwa AMRI yangu na **CHAPA** ya Mahakama leo hii tarehe ..................**Mwezi** .................**2024**

**NAIBU MSAJILI**
**KANDA YA DAR ES SALAAM**

**IN THE DISTRICT COURT OFDODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 5130 OF 2024**

**In the matter of the Estate of the late GRACE ROBERTH MAKANTA**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR APPOINTMENT OF ADMINISTRATIX OF A SMALL ESTATE BY ZEBADIAH EDWIN MAANGA**

**FORM 58**

**APPLICATION FOR APPOINTMENT OF ADMINISTRATIX OF SMALL ESTATE**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 15TH Day of APRIL, 2024

Dated at Dodoma this 13TH Day of MARCH, 2024.

..............................................
**RESIDENT MAGISTRATE**

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042,**

**DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO,MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

Kwa

## HABARI KIMATAIFA

# Biden, Trump rasmi uchaguzi Marekani

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani Joe Biden na mtangulizi wake Donald Trump watakabiliana tena katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu baada ya wote wawili kupata kura nyingi katika kuomba uteuzi wa kugombea nafasi ya urais.

Katika mikutano ya vyama wote idadi kubwa ya wajumbe imewachagua wote wawili kuwania nafasi hiyo katika uchaguzi utakaofanyika Novemba mwaka huu.

Wanachama wa Democtatic wanaoishi walishiriki kupiga kura ya maoni Jumanne iliyopita na wengi walimchagua Biden kupeperusha bendera ya chama chao.

**Rais Biden ambaye ana umri wa miaka 81, alisema ameheshimiwa na wapiga kura ambao wameunga mkono ombi lake la kuchaguliwa tena.**

Kutokana na matokeo hayo, wapiga kura wa Marekani watakabiliwa na uchaguzi utakaowakutanisha wanasiasa hao kama ilivyokuwa 2020.

Uteuzi rasmi katika chama hicho utafanywa katika kongamano litakalofanyika katika msimu wa joto.

Rais Biden ambaye ana umri wa miaka 81, alisema ameheshimiwa na wapiga kura ambao wameunga mkono ombi lake la kuchaguliwa tena.

Hata hivyo, tishio la nafasi yake lipo kwa Trump kuliko wakati wowote kutokana na kuongezeka kwa umaarufu wake.

Akitoa mfano wa mwelekeo chanya wa kiuchumi, alisema Marekani ilikuwa katikati ya kurejea nwenye nguvu yake,.



Trump



Biden

Alisema Marekani inakabiliwa na changamoto kwa mustakabali wake kama demokrasia, na kutoka kwa wale wanaotaka kupitisha vikwazo vya utoaji mimba na kupunguza programu za ustawi wa kijamii.

"Ninaamini kwamba watu wa Marekani watachagua kuendelea kwa uwepo wetu katika siku zijazo," alisema Biden.

Nafasi yake ya urais ilimweka Biden kifua mbele na hakukabiliwa na wapinzani wakubwa katika uteuzi wa chama chake.

Licha ya wasiwasi kutoka kwa wapiga kura kwamba umri wake mkubwa unapunguza uwezo wake wa kutekeleza majukumu ya urais, chama chake kilimuunga mkono.

Wakati huo huo, Trump, mwenye miaka 77, anaendelea kuwa kipenzi cha wapiga kura wa chama cha Republican, ambao wamesababisha ashinde katika kila mchujo dhidi ya wapinzani wake. **BBC**

## Putin atangaza yuko tayari kutumia nyuklia

**MOSCOW,** Rusia

RAIS wa Russia Vladimir Putin ametoa onyo kwa nchi za Ulaya kwamba iko tayari kutumia silaha za nyuklia ikiwa kutakuwepo tishio kwa serikali na uhuru nchi yake.

Putin ametoa onyo hilo kabla ya kufanyika kwa uchaguzi wiki hii, kiongozi huyo ana uhakika wa kujishindia muhula mwingine wa miaka sita madarakani.

Katika mahojiano na kituo cha televisheni cha serikali ya Russia yaliyotolewa hewani jana, Rais Putin alimuelezea kiongozi wa Marekani, Joe Biden kama mwanasiasa mkongwe anaelewa kikamilifu hatari zinazoweza kutokea ikiwa mzozo utatanuka.

Rais Putin, alisisitiza kuwa vikosi vyake vyenye dhamana ya silaha za nyuklia vimejitayarisha kikamilifu na kueleza kwamba mifumo ya silaha za nyuklia ya Russia ya angani, majini na ardhini ni bora Zaidi.

" Kwa mtazamo wa kijeshi na kiufundi, bila shaka, tuko tayari kwa vita vya nyuklia. Wanajeshi wa Russia daima wako katika hali ya utayari wa kupambana. Hili ndilo jambo la kwanza. Pili, kwa ujumla, mifumo yetu ya nyuklia ni ya kisasa zaidi kuliko mingine yoyote. Ni sisi tu na Marekani ambao tuna mifumo kama hii. Lakini mifumo yetu ni ya kisasa zaidi." Alisema.

Kiongozi huyo amekuwa mara kwa mara akielezea juu ya utayari wake wa kutumia silaha za nyuklia tangu alipoivamia Ukraine Februari mwaka 2022.

Aidha, rais huyo alisema ikiwa washirika wa Ukraine watatuma wanajeshi kuisaidia nchi hiyo iliyokumbwa na vita, hilo halitobadili matokeo katika uwanja wa vita kama ilivyokuwa kwa hatua yao ya kuipatia silaha.

Wakati huo huo, ndege zisizo na rubani za Ukraine zimelishambulia jengo la idara ya usalama ya Russia (FSB) katika mji wa mpakani wa Belgorod. **DW**



Baadhi ya Wapalestina wakipata msaada wa chakula kutoka kwa mashirika ya kibinadamu wanaotoa huduma eneo la Ukanda wa Gaza juzi. **PICHA: EPA**

## Marais Kagame, Tshisekedi kujadili amani

**LUANDA,** Angola

SERIKALI ya Angola imesema Rais wa Rwanda Paul Kagame, amekubali kukutana na kiongozi wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) Felix Tshisekedi, kujadili usalama mashariki mwa nchi hiyo.

Akizungumza na waandishi wa habari katika mji mkuu wa Angola wa Luanda, Waziri wa Mambo ya Nje, Tete Antonio, alisema tarehe rasmi ya viongozi hao wakuu kukutana itatangazwa na mpatanishi.

Tangazo hilo limekuja baada ya mkutano uliofanyika kati ya Rais Paul Kagame na rais wa Angola Joao Lourenco ambaye ni mpatanishi wa mgogoro huo aliyeteuliwa na Umoja wa Afrika.

Katika mkutano huo uliofanyika jijini Luanda, wakuu hao wa nchi walikubaliana kuhusu hatua muhimu za kushughulikia mizizi ya machafuko na haja ya kuendeleza michakato ya amani ya Nairobi na Luanda ili kurejesha amani na utulivu katika kanda hiyo.

Mwishoni mwa Februari, ikulu ya DRC kupitia ukurasa wake wa X, ilimnukuu Tete Antonio, ikithibitisha kwamba Rais Tshisekedi amekubali kukutana na rais wa Rwanda.

Hata hivyo, ilisema taarifa hiyo kuwa Rais Tshisekedi anataka kuona kabla ya mkutano huo na Rais Kagame, vikosi vya Rwanda viondoke katika ardhi ya DRC na iache kuwasaidioa waasi wa M23.

Wakati huo huo, msemaji wa Serikali ya Rwanda,Yolande Makolo, hajakanusha wala kukubali taarifa ya kuwepo kwa mkutano huo kwa viongozi hao wawili.

Radio Okapi inayofadhiliwa na Umoja wa Mataifa iliripoti kwamba Rais Tshisekedi na Kagame watajaribu kumaliza mzozo huo na kuondoa tuhuma za kila upande za kuwaunga mkono waasi.

"Rwanda daima imekuwa wazi kwa mazungumzo, na juhudi za kikanda za kutatua mzozo wa mashariki mwa DRC. Haitakuwa mara ya kwanza kwa Rais Kagame kukutana na Rais wa DRC," alisema Makolo

Mwezi uliopita wizara ya mambo ya nje ya Angola pia ilisema rais wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Felix Tshisekedi, amekubali kufanya mazungumzo ya moja kwa moja na Kagame

Angola imeombwa na Umoja wa Afrika kuwa mpatanishi kati ya nchi hizo mbili katika jaribio la kusitisha mapigano kati ya jeshi la Kongo na kundi la waasi la M23 Rwanda inatuhumiwa kuunga mkono M23, jambo ambalo inakanusha. **BBC**

# MKUNDA ATAKA UBINGWA LIGI BARA UHAMIE JESHINI

**Na Shufaa Lyimo**

MKUU wa Majeshi ya Ulinzi Tanzania, Jenerali Jacob Mkunda, amesema anatamani kuona timu zinazomilikiwa na taasisi hiyo zinatwaa ubingwa wa Ligi Kuu Bara, imeelezwa.

**Mkunda alisema amechoka kuona vigogo wa soka nchini, Simba na Yanga pekee kila msimu wanatwaa taji hilo na si vilabu vingine.**

Bosi huyo wa alisema hayo juzi usiku katika hafla ya uzinduzi wa Kamati Maalumu ya Uanzishwaji ya Vituo vya Michezo vya Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) na makabidhiano ya mabasi kwa timu za Mashujaa FC, JKT Tanzania zinazoshiriki Ligi Kuu Bara.

Pia mabingwa watetezi wa Ligi Kuu ya Soka ya Wanawake Tanzania, JKT Queens walikabidhiwa basi katika sherehe hizo zilizofanyika kwenye viwanja vya Klabu ya Gofu ya Lugalo, Dar es Salaam.

Alisema jeshi litashirikiana na viongozi wa klabu hizo kuhakikisha linarudisha hadhi ya timu za majeshi na kuwataka wazidishe juhudi katika mashindano yote wanayoshiriki.

Aliongeza kwa kuwataka wapambane na kuhakikisha hakuna timu itakayoshuka daraja.

"Natamani kuona siku moja timu za majeshi zinapata ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na sio Simba na Yanga pekee ndio zenye uwezo huo, naamini mkijituma ipo siku mtashika nafasi za juu," alisema Mkunda.

Aliongeza miaka ya nyuma Tanzania ilipata medali nyingi katika mashindano ya kimataifa ambazo zililetwa na timu za majeshi tofauti na miaka ya sasa jambo ambalo anataka warejeshe heshima.

Bosi huyo alisema pia amepokea mapendekezo kutoka kwa wadau mbalimbali wa michezo nchini ambayo yatasaidia kuimarisha timu zao na anaamini yametolewa na watu wenye uzoefu na hana wasiwasi na kilichowasilishwa.

Aliongeza jeshi hilo litaupatia pia timu ya Amani Queens basi ambalo litawasili nchini muda wowote kwa sababu mchakato wake unaendelea kufanyika na wahusika wanatakiwa kuwa na subira.

Naye Mkuu Mafunzo wa JWTZ, Meja Jenerali Ibrahim Muhona, alimpongeza Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, kutokana na juhudi anazoendelea kuzifanya za kuitangaza vyema nchi kupitia mpira wa miguu.

Muhona alisema mchezo wa soka unaendelea kufanya vyema na amezitaka mafanikio timu zote zinazoshiriki michuano mbalimbali ya kimataifa.

Naye Rais wa TFF, Wallace Karia, alisema ndoto yake ya kuanzisha vituo vya michezo itatimia kupitia vituo vya jeshi na kueleza asilimia 50 ya nyota watakaozalishwa katika kila kituo watakuwa ni wachezaji wa soka.

"Ile ndoto yangu ya kuanzisha vituo vya michezo inakwenda kutimia kwa sababu mpaka sasa vituo viwili vya michezo Kigamboni na Tanga vimekamilika, na ni miongoni vya vituo bora hapa nchini, nikiwa na lengo la kuibua vipaji vya vijana kwa kusababu michezo ni ajira pamoja na kujenga afya," alisema Karia.




Mshambuliaji wa Kitunda FC, Shabani Mbaraka (wa pili kulia), akiwania mpira dhidi ya wachezaji wa Kipera katika mechi ya kirafiki iliyochezwa kwenye Uwanja wa Shule ya Msingi Kitunda, Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Azam FC yazindua kadi mashabiki wake*

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Azam umezindua kadi ya shabiki wa klabu hiyo katika hafla maalumu iliyofanyika kwenye ofisi za timu yao zilizopo kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Meneja Masoko wa Azam Pesa, Tunga Ally, alisema zoezi hilo limechukua muda mrefu kwa sababu walitaka shabiki wa klabu yao wawe na kadi yenye ubora mzuri.

Alisema wamezindua kadi za aina tatu ambazo ni Platinum itakayouzwa Sh. 50,000 wakati Gold itapatikana kwa Sh. 25,000 na ya fedha itanunuliwa kwa Sh. 5,000.

"Zoezi limechukua muda mrefu sana kwa sababu tulikuwa tunataka kuwapa mashabiki wetu kadi ambazo zitakuwa na thamani kubwa na zoezi la usajili limeanza leo (jana)," alisema Ally.

Naye Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat', alisema zoezi hilo litawasaidia kujua idadi halisi ya mashabiki wao nchi nzima.

Popat alisema uongozi wa timu hiyo unaendelea na mikakati mbalimbali ya kuhakikisha wanatapa ushindi katika mchezo wao dhidi ya Yanga utakaochezwa Jumapili.

"Tumejipanga kuhakikisha tunapata pointi tatu katika mchezo wetu ujao dhidi ya Yanga, tukiwa na lengo la kupambana kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu," alisema Popat.

# Tukuyu Stars FC yailaza Tutes Hub

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA wa Tanzania Bara mwaka 1986, Tukuyu Stars, wamepata ushindi wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Mikoa baada ya kuichapa Tutes Hub ya Ruvuma bao 1-0 katika mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Sabasaba, mkoani Njombe juzi.

Hiyo ni mechi ya pili kwa timu hiyo yenye maskani yake jijini Mbeya iliyoko katika Kundi A ambayo mechi yake ya kwanza dhidi ya Don Bosco ya Iringa ililazimishwa sare ya bila kufungana.

Matokeo hayo yanaifanya Tukuyu Stars iliyozitikisa Simba na Yanga mwaka 1986, kabla ya wachezaji wake wengi kutimkia katika timu hizo kongwe msimu uliofuata hali iliyosababisha ishuke daraja baadaye, ishike nafasi ya pili katika msimamo wa Kundi A baada ya kufikisha pointi nne.

Hausing FC, timu iliyotolewa na Yanga katika michuano ya Kombe la FA kwa kuchapwa mabao 5-1 mwezi uliopita, inaongoza kundi hilo ikiwa na pointi sita na hii ni baada ya kuifunga Don Bosco mabao 2-1 kwenye uwanja huo huo.

Katika Kundi B wanaotumia Uwanja wa Tamco ulioko Kibaha, Pwani, Stand FC ya Mtwara ilitoka suluhu dhidi ya Gunners ya Dodoma huku Black Six ya Buguruni, Dar es Salaam ilifungwa bao 1-0 dhidi ya Moro Kids.

Matokeo hayo yanaifanya Moro Kids kuongoza katika Kundi B ikiwa na pointi sita, Gunners ikishika nafasi ya pili baada ya kujikusanyia pointi nne.

Katika michezo nyingine, Red Agles ya Lindi ilijikuta ikipoteza kwa mabao 2-1 dhidi ya Singida Cluster ya Singida, mechi ikichezwa pia kwenye Uwanja wa Tamco huku Veteran Middle Age ya Tanga ilipoteza kwa bao 1-0, mchezo wa Kundi C uliochezwa kwenye Uwanja wa Tanzanite Kwaraa, Manyara.

Mechi nyingine ya Kundi D iliisha kwa sare ya bao 1-1 kati ya Mambali Ushirikiano ya Tabora dhidi ya Friends Ranger ya Dar es Salaam, mchezo ukifanyika kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza.

Timu zinazofanya vizuri katika ligi hiyo zitapanda kucheza First League zamani Ligi Daraja la Pili katika msimu ujao.

**Katika Kundi B wanaotumia Uwanja wa Tamco ulioko Kibaha, Pwani, Stand FC ya Mtwara ilitoka suluhu dhidi ya Gunners ya Dodoma huku Black Six ya Buguruni, Dar es Salaam ilifungwa bao 1-0 dhidi ya Moro Kids.**

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

#### GYOKERES ALENGWA

ARSENAL imemfanya mshambuliaji wa Sporting Lisbon na Sweden, Viktor Gyokeres, 25, kuwa shabaha yao kuu msimu huu. Mchezaji huyo wa zamani wa Coventry ana kipengele cha kuuzwa cha pauni milioni 85 katika mkataba wake. ***(Football Transfers)***

#### LIVERPOOL YAIGOMEA BARCA

LIVERPOOL imeiambia Barcelona kuwa winga wa timu ya taifa ya Colombia, Luis Diaz, 27, ni sehemu ya mipango ya muda mrefu ya klabu hiyo na hatauzwa msimu huu wa joto. ***(Mirror)***

#### PACHO AZIVUTIA KLABU EPL

KLABU za Arsenal na Liverpool zinavutiwa na beki wa Ecuador na Eintracht Frankfurt, Willian Pacho, 22. ***(90min).***

#### BRIGHTON YAMWANIA REISS

WINGA wa Arsenal, Gyokeres Reiss Nelson, 24, anawaniwa na Brighton msimu wa joto. ***(Teamtalk)***

#### GREENWOOD KUPIGWA BEI

KLABU ya Manchester United inataka pauni milioni 43 kumuuza mshambuliaji wa England, Mason Greenwood, 22, ambaye yuko Getafe nchini Hispania kwa mkopo. Klabu ya Saudi Arabia ambayo haikutajwa jina imeonesha nia ya kutaka kumsajili Greenwood. ***(Mirror)***

#### MIKEL MERINO KUREJESHWA

MANCHESTER United inajaribu kumrejesha England kiungo wa zamani wa Newcastle United, Mikel Merino, 27. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania anaichezea Real Sociedad. ***(COPE)***

#### HERMOSO HUYO VILLA

LICHA kutakiwa na Juventus na AC Milan, ni Aston Villa ndio wako katika nafasi nzuri ya kumsajili beki wa Atletico Madrid, Mario Hermoso, 28, kwa uhamisho wa bila malipo msimu huu. ***(calciomercato.com)***

#### STERLING KUUZWA

CHELSEA huenda wakawauza wachezaji nyota kadhaa msimu huu, akiwamo mshambuliaji wa England, Raheem Sterling, 29. ***(Mail)***

#### GONCALVES AFUATILIWA

WEST Ham inamfuatilia kiungo mshambuliaji wa Sporting Lisbon na Ureno, Pedro Goncalves, 25. Mkataba wake na Sporting unaendelea hadi Juni 2027, lakini kuna kipengele cha kuachiliwa kwa pauni milioni 68. ***(Record)***

#### KUONGEZWA MKATABA

KLABU ya Manchester City ipo kwenye mazungumzo ya kuongeza mkataba na mlinda mlango wa Ujerumani, Stefan Ortega, 31, katika klabu hiyo. ***(Florian Plettenberg)***

#### WALKER AITAKA SAUDIA

MLINZI wa Manchester City na England, Kyle Walker, 33, amesema angependa kuhamia Saudi Arabia, ingawa kwa sasa hayuko tayari kuondoka Ligi Kuu England. ***(FIVE)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ARTETA ASHUTUMIWA KUITUKANA FAMILIA YA KOCHA WA FC PORTO

**LONDON,** England

### ●●● Conceicao alisema kocha huyo Mhispania aliwatusi watu wa familia yake wakati mchezo...

KOCHA wa FC Porto, Sergio Conceicao amemshutumu Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta kwa kuitukana familia yake wakati Waingereza hao juzi usiku wakishinda kwa mikwaju ya penalti dhidi ya timu hiyo ya Ureno na kujikatia tiketi ya kutinga robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara ya kwanza tangu 2010.

**Alipotakiwa kufafanua kilichotokea, Conceicao kupitia mkalimani wa Shirikisho la Vyama vya Soka Ulaya, Uefa alinukuliwa akisema, "Wakati wa mchezo na kuelekea benchi yeye, kwa Kihispania, sijui ndio ilivyo kwa makocha wa Hispania, aliitukana familia yangu.**

"Na kisha mwishoni, nilisema tafadhali usimtukane mtu ambaye hayupo hapa kati yetu, unapaswa kuzingatia mafunzo ya timu yako," alisema Conceicao.

Hata hivyo, vyanzo vya Arsenal viliiambia ESPN kwamba Arteta alikanusha vikali shutuma hizo.Washikabunduki walitinga hatua hiyo baada ya kupata ushindi wa penalti 4-2 baada ya bao la Leandro Trossard dakika ya 41 kusawazisha mchezo wa kwanza wa hatua ya 16 kwa uwiano wa bao 1-1 na kulazimisha mchezo kwenda muda wa ziada na baadaye changamoto ya mikwaju ya penalti.

Wendell na Galeno mikwaju yao ya penalti iliokolewa na David Raya, lakini makocha hao wawili waligombana tena wakati wa kipenga cha mwisho. Baada ya mechi, Arsenal na Arteta walikuwa na nia ya kuangazia usiku wa kihistoria ambapo hatimaye walimaliza msururu wa vipigo saba mfululizo katika hatua hiyo ya mashindano haya.

"Kwa timu kufanya hivyo wakati haijaweza kufanya hivyo kwa miaka 14, nawaambia ni nguvu," alisema Arteta.

"Mipaka ni mdogo sana, unatafuta njia ya kufanya tena. Naona wanataka kiasi gani, wanajaribu kiasi gani na wanaweza kujitolea chochote kushinda. Ukicheza hivi mwisho mambo mazuri yanaenda vizuri.

"Sasa nitakaa nyumbani, nitaangalia timu nyingine tunazopaswa kucheza na kuanza mlima mwingine mkubwa wa kupanda."

Hii haikuwa mara ya kwanza kwa Conceicao kugombana na kocha kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Alimshutumu kocha wa wakati huo wa Chelsea, Thomas Tuchel kwa kumtusi wakati The Blues walipoitoa Porto katika hatua ya robo fainali Aprili 2021.

Conceicao pia alitoa madai kama hayo kuhusu kocha wa Manchester City, Pep Guardiola kufuatia mchezo wa hatua ya makundi kwenye Uwanja wa Etihad Oktoba 2020.

Arsenal wameungana na Real Madrid, Manchester City, Barcelona, Bayern Munich na Paris Saint-Germain kwenye chungu cha droo ya robo fainali kesho Ijumaa, huku washindi wawili waliobaki walitarajiwa kupatikana jana wakati Borussia Dortmund ilipotarajiwa kucheza dhidi ya PSV Eindhoven na Inter Milna dhidi ya Atletico Madrid.

# SANCHO HATAKI KURUDI MAN UNITED



**DORTMUND,** Ujerumani

JADON Sancho amesema hana nia ya kurejea Manchester United huku akimlaumu Kocha Erik ten Hag kwa kusababisha kushuka kwa kiwango chake cha soka, kwa mujibu wa ripoti.

Baada ya kuachwa nje ya kikosi cha Man United kwa mechi ya nne za Ligi Kuu msimu huu, Sancho alikataa hadharani mapendekezo ya Ten Hag kwamba alifukuzwa kwa kukosa bidii katika mazoezi, na hivyo kusababisha uhamisho wa miezi minne ambao hatimaye ulisababisha arejeshwe kwa mkopo Dortmund katika dirisha la usajili la Januari.

Mkataba wa mkopo wa Sancho haujumuishi kipengele cha kudumu cha uhamisho na hivyo anatarajiwa kurejea United msimu wa joto, lakini kwa mujibu wa gazeti la Bild, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 tayari ameweka wazi kuwa hana nia ya kurejea Old Trafford.

Ripoti hiyo imedai Sancho amemlaumu Ten Hag na kuwa hana nia ya kufanya kazi tena chini ya Mholanzi huyo.

Ikiwa atafikiria kurejea chini ya kocha mpya haijulikani, lakini imani ni kwamba Sancho analenga kuendelea na Dortmund.

Tatizo la Sancho ni kwamba Dortmund kwa sasa hawawezi kumudu kumsajili kwa mkataba wa kudumu, ingawa wanataka kumsajili kwa mkataba mpya wa mkopo, hawawezi kulipa sehemu kubwa ya mshahara mkubwa wa winga huyo.

Maofisa wa Dortmund bado wanapanga kujaribu kusaini mkataba mwingine wa mkopo kwa Sancho, lakini wanaweza kuangalia uhamisho wa kudumu ikiwa United itaonesha nia ya kubadilishana.

Mshambuliaji Donyell Malen, ambaye ameripotiwa kupatikana kwa pauni milioni 43 msimu huu wa joto, anatajwa kuwa tegemeo katika harakati za Dortmund kumnyakua Sancho.

Baada ya kuanza maisha polepole kule Dortmund, Sancho alifunga bao lake la kwanza msimu huu katika ushindi wa 2-1 dhidi ya Werder Bremen wikendi iliyopita ambapo maofisa wa klabu hiyo walikiri kuwa bado anafanya kazi ya kurejea katika utimamu kamili.

# Davies agomea mshahara kiduchu Bayern



**MUNICH,** Ujerumani

BAYERN Munich imempa mlinzi wa kushoto, Alphonso Davies ofa ya mshahara mdogo kuliko alioomba wakati wakijaribu kumshawishi mchezaji huyo anayelengwa na Real Madrid kusaini mkataba mpya, kwa mujibu wa ripoti.

Davies amebakisha miezi 18 kwenye mkataba wake wa sasa na ameweka wazi kwamba hana mpango wa kubakia huko Bravia.

Sky Sport Germany iliandika kwamba mchezaji huyo wa kimataifa wa Canada mwenye umri wa miaka 23 ana pendekezo mezani kutoka kwa Bayern ambapo atalipwa mshahara wa mwaka kati ya euro milioni 11 na 13, sawa na hadi euro 250,00 kwa wiki, na mkataba huo utamalizika mwaka 2029.

Hata hivyo, Davies alitaka euro milioni 20 kwa msimu, jambo ambalo linaacha pande hizo kushindwa kufikia mazungumzo.

Zaidi ya hayo, Bayern wanaonekana kukataa kutimiza matakwa kama hayo na wamedokezwa kumpigia simu mchezaji huyo na kumwacha afanye mazungumzo na Real Madrid ikiwa atasisitiza kupata kiwango kama hicho.

90min ilifichua mnamo Novemba kwamba, Davies alikuwa tayari kujadili masharti mapya na Bayern, lakini anatafuta mshahara ambao anahisi unafaa na kiwango chake cha kimataifa.

Timu kama Manchester City, Liverpool, Chelsea na Paris Saint-Germain zote zinavutiwa na Davies, lakini mwishowe wanaamini kwamba ana nia ya kujiunga na Real Madrid na wana mashaka na uwezekano wao wa kumshawishi.

# Xavi: Barca imethibitisha haina mzaha Ligi ya Uefa

**BARCELONA,** Hispania

XAVI Hernández aliwajibu wakosoaji wake ambao anasema waliita 'Barcelona mzaha wa Ligi ya Mabingwa Ulaya', baada ya kuiongoza timu hiyo ya Katalunya kutinga robo fainali ya mashindano hayo kwa mara ya kwanza tangu 2020.

Fermín López, João Cancelo na Robert Lewandowski kila mmoja alifunga bao kwenye Uwanja wa Olympic Jumanne Barca ilipoilaza Napoli 3-1, na hivyo kufanikiwa kushinda kwa jumla ya 4-2 na kujikatia tiketi ya kutinga hatua ya nane bora.

Alisema Barca inawakilisha maendeleo makubwa katika kiwango cha Ulaya licha ya kushindwa kufuzu kutoka hatua ya makundi katika misimu miwili iliyopita na kufungwa na Paris Saint-Germain katika hatua ya 16 bora msimu wa 2020-21.

"Nilisema tungepiga hatua mbele kwa uamuzi wangu wa kwenda majira ya joto," alisema Xavi, ambaye mapema mwaka huu alitangaza kuachia ngazi mwishoni mwa msimu huu.

"Watu hawakuniamini, walisema ningepoteza muda kwenye chumba cha kubadilishia nguo. Tumepokea ukosoaji usio wa haki. Kumekuwa na shinikizo kubwa kwa wachezaji.

"Hata nilisoma kwamba tulikuwa mzaha wa Ligi ya Mabingwa Ulaya. Na sasa nini?"

Maneno ya Xavi yalikuja huku Barca wakiwa nyuma zaidi ya vinara wa LaLiga Real Madrid na kuondolewa kwenye Supercopa ya Hispania na Copa del Rey mnamo Januari.

Hata hivyo, bado ana nafasi ya kujiinua kwa mafanikio katika Ligi ya Mabingwa na anadai timu yake iko katika hali nzuri zaidi kuliko iliposhinda taji la LaLiga tangu mwaka 2019.

"Tunacheza vizuri zaidi kuliko mwaka jana," aliongeza baada ya Barça kuendeleza mbio zao za kutoshindwa katika mashindano yote hadi kufikia mechi tisa mpaka sasa.

"Tunaelewa baadhi ya mambo vizuri zaidi. Licha ya matokeo, kile ambacho timu hii inafanya kinastahili sifa nyingi. Ni wakati wa kujivunia na kuthamini kile tulichofanya.



# Yanga kuendeleza ubabe leo Ligi Kuu?

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha Yanga leo kinatarajiwa kushuka kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi kukabiliana na Geita Goldi kwenye mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mchezo huo umepangwa kuanza saa 2:00 usiku huku macho ya mashabiki na wadau wakitaka kuona kama mabingwa hao watetezi wataendeleza kasi ya ushindi kwenye michezo ya Ligi Kuu.

Yanga itakabiliana na Geita Gold siku chache ikitoka kupata ushindi mnono wa mabao 5-0 dhidi ya Ihefu kwenye uwanja huo huo huku Geita ikitoka kupata ushindi wa bao 1-0 ugenini dhidi ya Dodoma Jiji FC katika uwanja wa Jamhuri, Dodoma.

Kuelekea mchezo huo Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi amesema wamefanya maandalizi mazuri kuwakabili Geita Gold katika mchezo huo muhimu.

Alisema haijalishi watapata ushindi wa idadi gani ya mabao kikubwa wanahitaja pointi tatu.

“Bado sina uhakika wa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu licha ya timu yangu kuendelea kupata alama tatu, baada ya mchezo na Ihefu mara moja tukaanza kujiandaa na mchezo huu, naamini tutafanya vizuri,” alisema Gamondi.

Wakati Gamondi akisema hivyo, Kocha wa Geita Gold, Denis Kitambi alisema wameifuatilia Yanga kwenye michezo yao ya hivi karibuni na kujiandaa kuwakabili.

Alisema wamefanya maandalizi ya namna gani ya kuweza kujilinda na kushambulia katika mchezo wa leo kulingana na namna wapinzani wao watakavyokuja.

“Kwa jinsi ambavyo Yanga wanavyocheza Aziz Ki (Stephane) ndio tatizo la kwanza tuliloaanza kulifanyia kazi wakati wa maandalizi yetu, lakini pia kuna Mudathiri (Yahya) ambaye mara nyingi amekuwa akitokea nyuma, anacheza kiungo lakini anajukumu kubwa la kushambulia, hawa wote tunatakiwa kuwachunga,” alisema Kitambi.



Anasema wamejiandaa kukabiliana na wapinzani wao hao na kuhakikisha wanaondoka na pointi.

# BENCHIKHA AKATISHA KOZI KUJA KUWAKABILI AL AHLY

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba, Abdelhak Benchikha, ameamua kukatisha masomo yake na kurejea nchini kuanza mikakati ya kuikabili Al Ahly kwenye mchezo wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Taarifa za uhakika zilizoifikia Nipashe jana zinasema Benchikha aliondoka nchini kuelekea Algeria siku chache zilizopita kwa ajili ya kuhudhuria kozi ya juu ya ukocha, lakini baada ya kutangazwa droo ya robo fainali ameamua kukatisha kozi hiyo na kurejea nchini.

Mmoja wa viongozi wa klabu hiyo ameiambia Nipashe kuwa kocha huyo anatarajiwa kurejea nchini siku yoyote kuanzia leo na tayari ametoa maombi kwa uongozi kuipeleka timu hiyo Zanzibar kwa ajili ya kuweka kambi katika kipindi ambacho ligi itasimama kupisha mechi za kirafiki za kalenda ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Ulimwenguni (FIFA).



“Kocha atarejea mapema kuendelea na majukumu yake, katika michuano hii ya kimataifa Benchikha hana masihara tayari tumeshamfahamu mpinzani wetu na ameweka mikakati yake kuelekea mchezo huo.

“Moja ya mikakati yake ni kutumia kipindi cha michezo ya kimataifa kwa timu za taifa katika kalenda ya FIFA, ameomba kambi Zanzibar lakini ametaka kuwapo kwa michezo ya kirafiki kabla ya kuwakabili Al Ahly,” alisema kiongozi huyo ambaye hakutaka jina lake litajwe.

Simba kwa mara nyingine itaumana na mabingwa hao watetezi wa Ligi ya Mabingwa Afrika katika michezo miwili ya hatua ya robo fainali kuwania kutinga nusu fainali.

Katika michezo hiyo, Simba ambayo juzi ilifanikiwa kupata ushindi wa mabao 3-1 kwenye ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Singida Fountai Gate, itaanzia nyumbani kati ya Machi 29 na 30 kabla ya kwenda kurudiana nao kati ya Aprili 5 na 6 jijini Cairo.



Miss Tanzania 2022, Halima Kopwe (aliyeshika kipaza sauti), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu mashindano ya urembo ya dunia yaliofanyika India hivi karibuni na kushika nafasi ya 40, kulia ni Mkurugenzi wa Ukuzaji na Maendeleo ya Sanaa, Edward Busanga na kushoto ni Kaimu Mwenyekiti wa Kamati ya Miss Tanzania, Halima Rajabu. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Yanga yaahidi kulipiza kisasi*

INATOKA UKURASA 24

tumepokea droo iliyotolewa na tunaanza maandalizi yetu, benchi la ufundi litafanya kazi yake na uongozi utajipanga kuhakikisha tunafanya vizuri,” Hersi alisema.

Naye Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, alisema hakuna kinachoshindikana katika soka na yeye binafsi anaifahamu vyema Mamelodi Soundowns.

Gamondi alisema timu zote nane zilizofika hatua hiyo ni bora, hivyo hakuna mechi itakayokuwa nyepesi.

“Tutaandaa mbinu za kukabiliana nao, mchezo wa nyumbani ni mchezo muhimu zaidi kwetu, naifahamu Mamelodi vizuri, tupo tayari kukabiliana na tuna muda wa kujiandaa,” alisema Gamondi.

Endapo Yanga itafanikiwa kusonga mbele katika michuano hiyo, hatua ya nusu fainali itacheza dhidi ya mshindi wa jumla wa mchezo kati ya Esperance de Tunis ya Tunisia au Asec Mimosas ya Ivory Coast.

Timu nyingine ya Tanzania iliyofuzu kucheza hatua ya robo fainali ya mashindano hayo yanayoendeshwa na kusimamiwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), ni Simba na yenyewe katika hatua hiyo itakutana na Al Ahly ya Misri, Wekundu wa Msimbazi pia wakipangwa kuanzia nyumbani.

# Samatta atemwa Stars

INATOKA UKURASA 24

shot Town, England, Mohammed Hussein, Kennedy Juma (Simba) Novatus Miroshi (Shakhtar Donestk- Ukraine na Miano Danilo wa Villena CF ya Hispania.

Viungo ni Feisal Salum ‘Fei Toto’, Yahya Zaydi (Azam FC), Mudathir Yahya (Yanga),Morice Michael (RFK Novi Sad, Serbia),Himid Mao (Telaea El Gaish SC, Misri) na Tarryn Allarakhia kutoka Wealdstone ya England.

Washambuliaji ni Mzize, Saimon Msuva (Alnajmah FC, Saudi Arabia), Kibu Denis (Simba), Abdul Suleiman ‘Sopu’ (Azam FC), Ben Starkie (Ilstone Town- England) na Charles M’mombwa



anayecheza soka la kulipwa huko Australia.

Michezo

Alhamisi Machi 14, 2024

Nipashe




## Arteta ashutumiwa kutukana

UKURASA 21

# YANGA YAAHIDI KULIPIZA KISASI

●●● Yajipanga kutorudia kilichotokea 2001, Gamondi kumaliza 'kazi' nyumbani

**Na Faustine Feliciane**

SIKU moja baada ya kupangwa kwa ratiba ya mechi za hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, mabosi wa Yanga wamesema wanajipanga kuhakikisha yaliyotokea mwaka 2001 katika michezo yao dhidi ya Mamelodi Soundowns kutoka Afrika Kusini hayajirudii.

**Mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga watakutana na vigogo hao kutoka Afrika Kusini mechi ya kwanza wakianzia nyumbani kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa kati ya Machi 29 na 30, mwaka huu.**

Kumbukumbu zinaonyesha mara ya mwisho timu hizo zilikutana mwaka 2001 katika hatua ya kwanza ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na mechi ya kwanza ilichezwa Afrika Kusini na kumalizika kwa wenyeji kuondoka na ushindi wa mabao 3-2.

Katika mchezo wa marudiano uliochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza, Yanga walilazimishwa sare ya mabao 3-3 na hivyo kuondolewa katika michuano hiyo kwa jumla ya mabao 6-5.

Akizungumza na Nipashe jana, Rais wa Yanga, Hersi Said, alisema katika mpira hakuna kinachoshindikana, hivyo uongozi na benchi la ufundi wanajipanga vyema kuhakikisha wanaepuka yaliyowakuta miaka 23 iliyopita.

Hersi alisema Yanga haina hofu yoyote ya kukutana na mpinzani huyo kwa sababu wana wachezaji wenye viwango vizuri na benchi la ufundi imara na kwa sasa kazi yao ni kujiandaa vyema kuwakabili Wasauzi hao.

"Tunafahamu wapinzani wetu wana timu nzuri, timu inayofanya vizuri Afrika, lakini huwezi kubeza pia ubora wa kikosi chetu,

INAENDELEA UKURASA 23



Rais wa Yanga, Hersi Said

## Samatta atemwa Taifa Stars

**Na Saada Akida**

ALIYEKUWA Nahodha wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Mbwana Samatta, ameachwa katika kikosi cha wachezaji 23 kilichoitwa kwa ajili ya kujiandaa na mechi mbili za kimataifa dhidi ya Bulgaria na Mongolia, imefahamika.

Nyota mwingine aliyeachwa katika kikosi hicho ni golikipa, Beno Kakolanya.

Hata hivyo, mshambuliaji wa Yanga, Clement Mzize na beki wa kati wa Simba, Kennedy Juma, wamerejea katika kikosi hicho.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Kaimu Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Hemed Suleiman 'Morocco' alisema timu hiyo inatarajia kuingia kambini Jumapili ili kuanza maandalizi ya michezo hiyo miwili ya kirafiki.

Morocco alisema wachezaji walioitwa katika kikosi hicho ni mchanganyiko wa vijana na nyota wenye uzoefu wa kuitumikia timu hiyo.

Alisema kikosi hicho kitaondoka nchini Machi 18, mwaka huu na kuanza safari ya kuelekea Azerbaijan ambapo michezo hiyo miwili ya kirafiki inayotambuliwa na Kalenda ya FIFA itachezwa.

"Tutakuwa na mechi mbili za kirafiki, tutacheza Machi 22 na Machi 25, mwaka huu dhidi ya Bulgaria na Mongolia, baada ya hapo wachezaji watarejea nchini haraka kwa ajili ya majukumu mengine.

Tumechanganya baadhi ya wachezaji ili kuwapa nafasi vijana na sura mpya kwa lengo la kutengeneza timu imara ijayo," alisema Morocco.

Kikosi kamili cha Stars ni makipa; Aishi Manula (Simba), Aboutwalib Mshery (Yanga) na Kwesi Kawawa (Syrianska FC, Sweden) wakati mabeki ni pamoja na Bakari Mwamnyeto na Ibrahim Bacca wote kutoka Yanga, Lusajo Mwaikenda (Azam FC), Haji Mnoga (Alder-

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >